# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Juni 23, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581716

www.ippmedia.com

0745 700710 LIKE & FOLLOW US

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com


UKURASA WA 2

**Maaskofu** Katoliki wachagua viongozi wapya, Katibu Mkuu aongezwa miaka mitatu



UKURASA WA 7

**Mbunge** apokewa kwa mabango msibani, adai ni mbinu za 'maadui'

UKURASA WA 11

MAISHA YALIVYO

**Mke** simtaki, watoto wangu ninawachukua




**PULISIC: MAREKANI IKO TAYARI COPA**

UKURASA 22

# Matobo ya bajeti

• **ACT** yaikosoa haijibu changamoto za wananchi; yadai kikokotoo bado tatizo...

*Endelea Ukurasa wa 3*



Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe (kulia) na Makamu wake (Bara), Tundu Lissu, wakiwa katika mkutano wa chama hicho uliofanyika Kansay, Karatu mkoani Arusha jana. Kulia ni wafuasi wa chama hicho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

## Lissu aanika mkakati CHADEMA kuvuna kura nyingi vijijini

UKURASA 5




Rais, Samia Suluhu Hassan, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mkutano na mgeni wake, Rais wa Jamhuri ya Guinea-Bissau, Umaro Sissoco Embalo (kushoto) Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Samia, Rais Guinea Bissau wakubaliana kutoa fursa tele

UKURASA 2

**MICHEZO** **USAJILI WA CHAMA SINEMA ILE ILE** UK.24 **KATUNI** UK.6

# TEC yachagua viongozi wapya

**Na Jenifer Gilla**

BARAZA la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) limewachagua Askofu wa Jimbo Katoliki Lindi, Wolfgang Pisa kuwa Rais wake na Askofu wa Jimbo la Katoliki Mpanda, Eusebius Nzingilwa kuwa Makamu wa Rais.

Vilevile, limemchagua kwa awamu ya tatu Padri wa Jimbo Katoliki Singida, Charles Kitima kuwa Katibu Mkuu wa baraza hilo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi kwa umma na Rais wa TEC aliyemaliza muda wake, Askofu Mkuu Gervas Nyaisonga, katika Misa Takatifu ya shukrani kwa kupata uongozi mpya iliyoadhimishwa Kanisa la Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya Asili, Makao Makuu ya TEC, Kurasini Dar es Salaam, viongozi hao watahudumu kwa kipindi cha miaka mitatu.

Alitaja viongozi wengine ni Padri Chesco Msanga aliyeteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu, Askofu Mkuu Issack Amani aliyeteuliwa kuwa Mwenyekiti Kurugenzi ya Uchungaji na Askofu Nzigilwa ambaye pia anakuwa Mwenyekiti wa Kurugenzi ya Mawasiliano.

Wengine ni Askofu Augustine Shao aliyeteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kurugenzi ya Ukaguzi na Askofu Henry Mchamungu katika nafasi ya Mwanasheria wa Baraza.Alimpongeza Rais mpya na safu yake kwa kuaminiwa na baraza hilo na kuwashukuru watendaji wote wa sekretarieti na kuomba radhi pale palipotokea kasoro katika kipindi cha uongozi wake.

Askofu Pisa alishukuru Mungu na maaskofu kwa kumteua kushika nafasi hiyo na kusisitiza kuwa yeye na wenzake na wako tayari kutekeleza majukumu.

Pia alimpongeza na kumshukuru Askofu Mkuu Nyaisonga na Makamu wake, Askofu Flavian Kassala kwa kazi kubwa waliyofanya na kuahidi kuendeleza pale walipoishia na kuomba ushirikiano na mwongozo kila watakapohitaji kutoka kwao.

### KUHUSU WOLFGANG

Kwa mujibu wa wasifu uliowekwa kwenye tovuti ya Vatican, Askofu Wolfgang alizaliwa Julai 6, 1965 Karatu, Jimbo Katoliki la Mbulu. Alipata masomo na malezi ya kitawa Lusaka, Zambia na Chuo Kikuu Kishiriki cha Jordan, Morogoro.

Aliweka nadhiri za daima Agosti 15, 1998 na kupewa Daraja Takatifu la Upadri Septemba Mosi 1999.

Kati ya mwaka 2005 na 2008, aliteuliwa kuwa Gambera wa Seminari Ndogo na baadaye alijiendeleza zaidi katika masomo ya maadili Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Marekani na mwaka 2011 akachaguliwa kuwa Mkuu wa Shirika la Wakapuchini Kanda ya Tanzania na kuwaongoza hadi mwaka 2017.

Mwaka 2017 hadi 2019, alirejea katika chuo cha maadili ya kikatoliki na kujipatia Shahada ya Uzamili katika Maadili na aliporudi aliendelea kufanya shughuli za kichungaji parokiani Kibaigwa hadi alipoteuliwa na Baba Mtakatifu Francisko kuwa Askofu mpya wa Jimbo Katoliki la Lindi Aprili 9, 2022.

### KUHUSU NZINGILWA

Mhashamu Askofu Nzigilwa alizaliwa Agosti14, 1966, mkoani Mwanza. Alipewa Daraja ya Ushemasi katika Kanisa Kuu la Mtakatifu Yosefu Januari 6, 1995 na Daraja ya Upadri Juni 23, 1995.

Januari 28, 2010, Baba Mtakatilfu Benedikto XVI alimtangaza kuwa Askofu Msaidizi wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam. Aliwekwa Wakfu kuwa Askofu Msaidizi kwenye Viwanja vya Msimbazi Centre Machi 19, 2010. Mei 13, 2020, aliteuliwa kuwa Askofu Msaidizi wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam na Mtakatifu Francisko, akichukua nafasi iliyoachwa wazi na Mhashamu Askofu Mkuu Gervas Nyaisonga, baada ya kuhamishiwa Jimbo Kuu la Mbeya mwaka 2019.

### KATIBU MKUU TEC

Padri Kitima baada ya kutoka masomoni alipelekwa Chuo cha Nyegezi, kikiwa katika mchakato kuwa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT), lakini baadaye alikuwa mkuu wa chuo wa pili, kisha kuingia TEC ambako amehudumu kwa miaka sita.

Ndiye aliyetajwa kuhusika kwa kiasi kikubwa na upanuzi na ukuaji wa chuo kikuu hicho (SAUT).



Naibu Balozi wa India nchini, Manoj Verma (kushoto) akiagana na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Christina Mndeme muda mfupi baada ya kumaliza mazungumzo baina yao yaliyofanyika katika Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma Juni 20 mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia, Rais wa Guinea Bissau wakubaliana kutoa fursa lukuki

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan na mgeni wake, Rais wa Jamhuri ya Guinea-Bissau, Umaro Sissoco Embaló, wamejadiliana mambo mbalimbali yaliyojikita katika uchumi, uhusiano wa kikanda na kimataifa pamoja na ulinzi na usalama barani Afrika ili kukuza zaidi ushirikiano kati ya nchi zao.

Viongozi hao pia wameshuhudia utiaji saini Mkataba wa Mwongozo wa Ushirikiano baina ya nchi hizo uliofanywa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Januari Makamba na Waziri wa Mambo ya Nje na Uhusiano wa Kimataifa na Jamii wa Guinea-Bissau, Carlos Pinto Pereira.

Baada ya mazungumzo yao ya faragha Ikulu jijini Dar es Saalam jana, Rais Samia aliwaambia waandishi wa habari kuwa walijadili namna ya kukuza biashara, uwekezaji na kuimarisha ushirikiano katika sekta ya kilimo, hususani zao la korosho.

Rais Samia alisema walirejea adhma ya bara hilo ya kufungua eneo huru la biashara na kuhakikisha wanalitumia ipasavyo kwa kuanza kuchukua hatua za makusudi, ili kukuza biashara na uwekezaji kati yao kwa ushirikiano katika zao la korosho kwa kufanya utafiti na kuongeza thamani.

"Bara letu liko mbioni kuhakikisha Eneo Huru la Biashara Afrika linafunguka, lengo letu likiwa kukuza zaidi kiwango cha biashara kati ya nchi za Afrika.

"Kuanzishwa soko hilo pia kutachochea ukuaji wa viwanda, uingizaji thamani wa mazao yetu pamoja na kuleta ajira kwa vijana wetu. Tumezungumza (Tanzania na Guinea-Bissau) mambo mengi yenye lengo la kukuza zaidi uhusiano na ushirikiano kati ya mataifa yetu mawili.

"Tulijikita zaidi katika nyanja za kiuchumi, pia tumebadilishana mawazo kuhusu masuala muhimu ya kikanda na kimataifa ikiwamo ukuzaji amani na usalama barani Afrika," Rais Samia alisema.

Mkuu wa Nchi alisema wamekubaliana pia kushirikiana na nchi zingine za Afrika kuhakikisha bidhaa za kilimo zinapata bei nzuri kwa kutengeneza umoja na kuwa na sauti katika soko la dunia.

Eneo lingine waliojadili ni namna watakavyoshirikiana kutumia fursa zinazopatikana katika uchumi wa bluu (uvuvi, utalii na ushafirishaji) kwa kuwa nchi hizo zina eneo kubwa la mwambao, hivyo kuwaweka katika nafasi nzuri ya kufanya biashara na nchi zinazowazunguka.

Vilevile, Rais Samia alisema wamekubaliana kuendelea kushauriana na kushirikiana katika kushughulikia changamoto mbalimbali za kiusalama barani, likiwamo tishio la ugaidi na biashara haramu ya dawa za kulevya.

"Ziara hii ni fursa kwa nchi zetu kukuza na kuimarisha uhusiano na ushirikiano kati yetu. Kama mnavyofahamu, mataifa yetu mawili yana uhusiano mzuri ambao umedumu kwa muda mrefu. Uhusiano kati ya watu wetu umedumu hata kabla ya nchi zetu hazijapata uhuru," Rais Samia alisema.

Aliitaja ziara ya mgeni wake huyo kuwa ya kihistoria kwa kuwa ni mara ya kwanza kwa Rais huyo kutembelea Tanzania na ni fursa muhimu katika kuimarisha uhusiano ulioanzishwa na Marais wa kwanza wa nchi hizo, Hayati Julius Nyerere wa Tanzania na Luís Severino de Almeida Cabral wa Guinea Bissau.

Rais Umaro Sissoco Embaló alisema nchi hizo zikifanya kazi kwa pamoja kubadilishana uzoefu, zitachangia kufikia ajenda ya Afrika Tunayoitaka 2063 - kuwa na amani ya kudumu, ustahimilivu wa kisiasa, kuleta maendeleo endelevu na kujenga mataifa yenye ustawi.

Alikaribisha Watanzania wanaojihusisha na sekta binafsi kutembelea nchi hiyo, ili kujifunza biashara katika nyanja mbalimbali.

Nchi yake inaweza kuwa mlango wa kuingilia nchi zingine za Afrika Magharibi kupitia Mkataba ya Eneo Huru la Biashara la Afrika.

Alisema nchi hizo mbili zilishirikiana kuondoa ukoloni na ubaguzi, shughuli iliyofanywa na Kamati ya Ukombozi ua Umoja wa Afrika iliyokuwa na makazi yake Dar es Salaam.

Alisema mataifa ya Afrika yana jukumu muhimu kufanya kazi pamoja na kuandaa mustakabali wa dunia kwa kuwa yana rasilimali nzuri na uongozi sahihi unaoweza kuleta ustaarabu mpya.

Rais Umaro Sissoco Embaló yumo nchini kwa ziara ya siku tatu kuanzia juzi. Pamoja na mambo mengine, alitarajiwa kutembelea viwanda, Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) na Reli ya Kisasa (SGR).

## HABARI KITAIFA

MATOBO YA BAJETI

# ACT yasema bajeti haijibu changamoto za wananchi

**Na Halfani Chusi**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimesema bajeti ya serikali inayopendekezwa kwa mwaka ujao wa fedha, haijibu changamoto sugu zinazokabili wananchi na ipo kimatabaka.

Hayo yalisemwa jana mkoani Dar es Salaam na Kiongozi wa Chama hicho, Dorothy Semu wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uchambuzi wa bajeti inayopendekezwa uliofanywa na chama hicho.

Alisema bajeti ya serikali inayopendekezwa haijagusa kikamilifu kilio cha kikokotoo kwa wastaafu licha ya serikali kupendekeza kuongeza kutoka asilimia 33 hadi 40 kwa kundi la watumishi wa umma walio chini ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) huku kundi la Shirika la Taifa la Hifadhi ya Taifa (NSSF) likiwa na pendekezo la kuongezwa kutoka asilimia 33 hadi asilimia 35.

Alisisitiza kwamba kilio cha wastaafu wengi kinaitaka serikali irejeshe kikokotoo cha mafao cha awali cha asilimia 50 ya mafao ya mkupuo na hivyo wengi hawajafurahia ongezeko hilo.

Alisema bajeti pendekezwa pia haijagusa maisha ya Watanzania kwa kuwa walio wengi wako katika maisha magumu kutokana na kupanda kwa gharama za maisha kutokana na kodi na tozo.

"Bajeti haijibu changamoto za Watanzania, kila inapotangazwa bajeti inakuwa si ya kuwaletea wananchi unafuu wa maisha, bajeti iliyowasilishwa bungeni inaonekana imejikita zaidi katika kulipa madeni na posho za viongozi serikalini kuliko kuboresha maisha ya Watanzania maskini kwa kuwaboreshea barabara, umeme, maji na sekta za afya na elimu," alisema Dorothy.

Kiongozi huyo alisema chama hicho kimeamua kuionesha serikali upungufu huo kwa maslahi mapana ya Watanzania ili kusaidia kupata bajeti itakayojibu changamoto za wananchi.

Waziri Mkuu Kivuli wa ACT Wazalendo, Isihaka Mchinjita alisema mapendekezo ya bajeti hiyo yamejikita katika kulipa madeni na posho za watawala na hayajagusa kikamilifu huduma bora za afya, elimu, nishati, mafuta na gesi asilia.

Pia alizitaja sababu ya serikali kushindwa kukusanya fedha na hatimaye kuangukia katika madeni na kuongeza tozo kuwa ni pamoja na rushwa, utoroshwaji mkubwa wa madini nchini, mikopo ya misaada ambayo serikali inakuwa haina uhakika wa kuipata na yenye masharti na riba kubwa, pamoja kukosa ubunifu wa kutawanya wigo wa vyanzo vya mapato.

"Tulijaribu pia kuangalia fedha za bajeti kwa mwaka 2024/25 ni Sh. trilioni 49 zinakwenda wapi? Tukagundua mgawanyo wa matumizi unaonesha Sh. trillion 34.6 imetengwa kwa ajili ya mshahara, posho, magari, misafara ya viongozi, chai ambayo ni sawa na asilimia 70 ya bajeti.

"Miradi ya barabara, mikopo ya wanafunzi, ujenzi wa madarasa, dawa, pembejeo za kilimo maji Imetengewa Sh. trilion 14.7 sawa na asilimia 30. "Hii inaonesha Watanzania wenye kipato cha chini wanaendelea kuumia kwa kukosa huduma za msingi," alisema Mchinjita. Waziri Kivuli wa Fedha, Mipango na Hifadhi ya Jamii wa ACT Wazalendo, Kiza Mayeye alisema Deni la Taifa limeongezeka, hali aliyodai inahatarisha usalama wa nchi.

Alisema mpaka Aprili mwaka huu, Deni la Taifa liliongezeka kutoka Sh. trilion 82.25 ya mwaka 2023 hadi kufikia kufikia Sh. trilion 91.7 sawa na ongezeko la Sh. trilion 12.6 (asilimia 15.9).

Alisema kuna jambo baya katika ukopaji nchini kwa kuwa fedha zilizokopwa zinaendesha miradi kwa hasara, akikumbushia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere inaonesha kuna ubadhirifu wa fedha zinazotokana na mikopo hiyo. Pia alishauri magari ya serikali yatumie gesi asilia badala ya kuagiza mafuta kutoka nje ya nchi, akisisitiza hiyo itasaidia kupunguza gharama.

"Bajeti ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), ukiisikiliza haijielekezi kutatua changamoto ya upungufu wa walimu, kila utakapokwenda utakuta shule haina walimu wa kutosha, kuna unafuu kwa shule za mijini, vijijini ndiko balaa, tatizo hili linazidi kukithiri kila mwaka.

"Ukiiangalia bajeti ya serikali haijatenga fedha kwa ajili ya kuajiri walimu wengi, tuna vijana ambao wamemaliza vyuo hawana ajira, kila unapokwenda kwenye vijiji madarasa ni shida, watoto wanakaa chini, wazazi wanachangishwa fedha kujenga madarasa wakati hiyo ni kazi ya serikali," alisema.

Hata hivyo, Ibara ya 8(1)(d) ya Katiba ya nchi inaeleza wananchi kushiriki shughuli za serikali yao.

Waziri Kivuli huyo aliendelea: "Ukiangalia gharama za matibabu, mtu asiyekuwa na uwezo, kufa ni rahisi kwa sababu hana uhakika wa kupata matibabu bora.

"Tumeona Watanzania wanapoteza maisha kwa kukosa fedha za kujihudumia katika zahanati zetu, unakuta kuna nesi mmoja au wawili bado, kuna changamoto ya huduma za afya."

Vilevile alishauri serikali kuangalia uwezekano wa kuongeza viwanda vya kuzalisha sukari, ili kuondoka na uhaba wa bidhaa hiyo, akikumbushia kuwa mwishoni mwaka jana iliadimika mpaka kufikia kiwango cha kilo moja kuuzwa kwa Sh. 4,000 mpaka 5,000.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian



Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Dorothy Semu, akizungumza wakati wa mkutano wa uchambuzi wa bajeti ya serikali mwaka 2024/25, Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Airtel yaboresha huduma za intaneti

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Airtel Tanzania imeanza rasmi kutumia mkongo wa mawasiliano unaopita baharini wa 2Africa wenye uwezo mara 10 zaidi ya uliopo, ikiutaja utamaliza changamoto ya kukosekana huduma ya intaneti kwa sababu ya kukatika.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa na Airtel Tanzania jana, mkongo huo wenye urefu wa kilomita 45,000 unanganishwa mabara matatu ili kutoa huduma za intaneti ya kasi zaidi na hivyo kukuza uchumi wa kidijitali.

Ilielezwa katika taarifa hiyo kuwa hatua hiyo italeta maendeleo makubwa katiak kupanua na kuimarisha miundombinu ya kidijiti nchini.

"Mkongo huu wa kisasa wa 2Africa unaopita chini ya bahari na kusimamiwa na Airtel Tanzania utaiweka Tanzania katika viwango vya juu vya mabadiliko ya kukua kwa huduma za kidijitali, na kukidhi mahitaji ya uchumi wa nchi unaoendeshwa na huduma za mtandao," inasomeka sehemu ya taarifa hiyo.

Mkongo wa 2Africa hivi sasa umeanza rasmi kuhudumia kampuni ya teknolojia ambayo sasa inapokea masafa ya uwezo wanaohitaji kupitia kituo cha Airtel Cable Landing Station kilichoko Dar es Salaam (Mbezi Beach), kilichozinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan Agosti 10 mwaka 2023.

"Mkongo mpya wa Airtel 2Africa unakuwa suluhisho la pekee na ulinzi wa mikongo au kebo zingine za mawasiliano zinazopita chini ya bahari nchini," inabainishwa zaidi katika taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa uzinduzi huo wa Airtel Tanzania umekuja wakati mwafaka, hasa kutokana na kukatika kwa nyaya za mkongo wa mawasiliana unaopita chini ya bahari hivi karibuni, ambazo ziliathiri baadhi ya maeneo ya Afrika Mashariki, ikiwamo Tanzania.

Vilevile, ilielezwa katika taarifa hiyo kuwa mkongo huo utasaidia kuanzishwa vituo vya kuhifadhi kumbukumbu kieletroniki ili kukidhi ongezeko la shughuli za kidijiti nchini kutokana na kuboreshwa matumizi ya mtandao katika uhamishaji maudhui na kuhakikisha kasi ya juu ya 4G na 5G kwa watumiaji.

Airtel inaeleza katika taarifa yake hiyo kuwa mkongo wa mawasiliano wa 2Africa unaunganisha Tanzania na maeneo 43 duniani, na unahudumia zaidi ya watu bilioni tatu na kukuza muunganiko wa kimataifa wa wafanyabiashara kidijiti.

"Mkongo huu Tanzania utafanikiwa kuendeleza biashara ya mtandaoni na utawala wa kidijitali. Mkongo huu unaunga mkono mipango ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ikiwamo mipango ya maabara ya akili mnemba (Artificial Intelligence) na maabara za roboti.

"Ujio na kuwapo mkongo wa mawasiliano wa baharini wa 2Africa umefanikiwa kuwa nchini kutokana na maono ya uongozi wa Rais Samia na Waziri wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ya Habari, Nape Nnauye.

"Mkongo wa 2Africa unaifanya Tanzania kuwa kitovu na lango la kusambaza huduma kidijiti kimataifa, kukuza fursa za kiuchumi na maendeleo ya kiteknolojia," Airtel inafafanua katika taarifa yake hiyo.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA), Dk. Jabiri Bakari alisema mkongo huu mpya wa mawasiliano wa 2Africa unaopita baharini utachochea na kuboresha zaidi huduma bora za intaneti nchini.

"Mkongo huu mpya utakuwa msaada mkubwa katika kukabiliana na mhitaji ya huduma za mtandao wa intaneti nchini, ambazo mahitaji yake yamekuwa yakiongezeka maradufu kila baada ya miaka miwili.

"Nina hakika kuwa teknolojia hii itapelekea utekelezaji wa haraka wa mkakati wetu wa kuhimiza matumizi ya TEHAMA katika sekta zote na kuboresha uchumi wa kidijitali ambao Tanzania inatamani kufikia," alisema Dk. Bakari.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo Agosti mwaka huu, Rais Samia alisema Kituo cha 2Africa Cable Landing Station kinaashiria hatua muhimu na mustakabali wa nchi kupaa kidijiti na kwamba miundombinu si tu italeta mapinduzi katika huduma za mawasiliano, bali pia itaharakisha ukuaji uchumi kwa kuimarisha muungano na mataifa mengine.

Mkurugenzi Mkuu wa Airtel Tanzania, Dinesh Balsingh, alisisitiza kwamba mazingira wezeshi ya serikali katika kupatikana kwa leseni pamoja na kuwapo mfumo bora wa udhibiti ndio sababu zilizowezesha Airtel Tanzania kuzindua kituo chao cha Airtel 2Africa kabla ya nchi nyingine.

# ZIC yakabidhi msaada wa vitabu vya mitaala sekondari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Bima la Zanzibar (ZIC) limekabidhi msaada wa vitabu vya mitaala kwa shule za sekondari kwa kushirikiana na Taasisi ya Mwanamke Initiatives Foundation (MIF).

Lengo la msaada huo ni kukuza kiwango cha ufaulu katika Shule za Mkoa wa Kusini Unguja, Zanzibar. Ulitolewa juzi makao makuu ya shirika hilo huko Maisara, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Akizungumza katika hafla hiyo, Kaimu Mkurugenzi wa ZIC, Jape Ussi alisema elimu ndiyo msingi wa maendeleo katika nchini na ni jukumu la kila mmoja kuunga mkono jitihada za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi kuendeleza upatikanaji elimu bora kwa watoto.

"Katika kuendeleza upatikanaji wa elimu bora kwa watoto wetu ZIC tunaahidi kuendelea kushirikiana na taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali katika kuona malengo ya viongozi wetu yanafanikiwa katika sekta ya elimu Zanzibar," alisema.

Alisema ni jukumu la kila mmoja kuona kuwa elimu inakuwa vizuri na wanafunzi wanafaulu katika mitihani yao ya taifa, ili kuwa viongozi wazuri wa baadaye.

Kaimu Mkurugenzi huyo alisema katika kusherekea miaka 55 ya shirika hilo, wameona fahari kushirikiana na Wizara ya Elimu kuwapatia vitabu vya mitaala kwa wanafunzi wa Zanzibar.

Alisema serikali inafanya jitihada kubwa katika kuhakikisha wanafunzi wote wa Zanzibar wanapata elimu iliyokuwa bora kulingana na mahitaji ya dunia yaliyopo hivi sasa.

Alisema kuwa katika kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu bora shirika hilo litaendelea kuunga mkono katika kutatua changamoto za kupata elimu kwa wanafunzi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mwanamke Initiatives Foundation (MIF), Sabra Mohamed alishukuru shirika hilo kwa kuchangia vitabu vya mitaala kwa ajili ya shule za sekondari katika Mkoa wa Kusini Unguja.

"Moja ya vipaumbele vyetu kama Taasisi ya Mwanamke Initiatives Foundation ni kuhakikisha tunasaidia jitihada za kuimarisha upatikanaji elimu bora katika nchi yetu, ikiwamo kuweka miundombinu imara na endelevu kwa vijana wetu ili waweze kufikia malengo yao pamoja na malengo ya nchi yetu kwa ujumla," alisema.

Sabra alisema kupatikana msaada wa vitabu hivyo kunalenga kuondosha sifuri kwa wanafunzi wa Mkoa wa Kusini.

Hafla hiyo ya makabidhiano inakwenda sambamba na maadhimisho ya miaka 55 ya Shirika la Bima la Zanzibar tangu kuanzishwa kwake Juni 20, 1969.

Hafla hiyo pia ilihudhuriwa na Mwakilishi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar pamoja na watendaji kutoka ZIC.



Moja ya vituo vya mabasi ya Mwendokasi kikiwa katika matengenezo Vingunguti, jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

# Lissu aanika mkakati wa CHADEMA kuvuna kura nyingi vijijini

**Na Godfrey Mushi,**
KARATU

MAKAMU Mwenyekiti wa CHADEMA Bara, Tundu Lissu, amesema majukumu waliyonayo kwa sasa, yeye na Mwenyekiti wake, Freeman Mbowe, ni kuruka anga kwa anga "kumalizana vijijini" na Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu.

Lissu pia ametoa angalizo kwa maofisa watendaji wa vijiji (VEO) watakaoengua wagombea wao katika mchakato huo wa uchaguzi, akihadharisha kuwa "hawatabaki salama".

Akizungumza jana na wananchi wa Mang'ola na Kata ya Eyasi, wilayani Karatu, mkoani Arusha, Lissu alisema:

"Tuna miezi minne tu ya kujipanga na kumalizana nao vijijini kwenye nafasi ya Mwenyekiti wa Kijiji, Kitongoji na Wajumbe wa Halmashauri za Vijiji. "Tukiwamaliza huku chini, tumewakata miguu, hawatainuka mahali popote. Mmenielewa, mmenipata?

"Mimi ninasema mchana kweupe. Ofisa Mtendaji wa Kijiji atakayeengua mgombea wetu yeyote; hawa watendaji wanakaa wapi, si wanakaa na sisi mitaani huku? Akiengua mgombea wetu mwambieni kabla hatujafika huko, ukiengua mgombea wetu hubaki.

"Achilia mbali kuwa Mwenyekiti wa Kijiji au Kitongoji, ninataka tushindwe kwenye kura tu. Tunataka wananchi watukatae kwenye kura tu, tusishindwe mezani, tusishindwe kwa wagombea wetu kuenguliwa."

Lissu pia alisema kwa sasa wanalo jukumu kujipanga kwa mwaka ujao, warudishe alichoita "heshima ya Karatu na heshima ya Mang'ola" na uchumi wake.

Wakati Lissu akiweka msimamo huo wa uchaguzi ujao katika serikali za mitaa, vijiji na vitongoji, Mbowe, Mwenyekiti wa CHADEMA hicho, alisema ukipita juu angani unaona umaskini wa Mang'ola na Eyasi.

"Watu wa Mang'ola na Eyasi mmepakana na Ngorongoro, mmepakana na Manyara, mbuga za wanyama, mmepakana na mbuga nyingine kule ya Tarangire.

"Ni watu ambao Mungu amewaweka katikati ya neema. Wilaya ya Karatu ina kilomita za mraba 3,000, kuna ardhi ya kulima zaidi ya kilomita za mraba 1,000, kuna hifadhi za misitu, kuna mbuga za wanyama; yaani ninyi watu wa Mang'ola, Eyasi ni watu mliopewa baraka.

"Inawezekana watu wa Eyasi hamwelewi. Hapo Ngorongoro, hapo Serengeti huwezi kwenda Serengeti bila kupita Karatu. Hapo mbugani hapo, kuna watu wanalala chumba siku moja kwa Dola za Kimarekani 5,000. Sijui mnanielewa?

"Dola za Marekani 5,000 ukizidisha mara Sh. 2,800 za Tanzania, piga hesabu utajua watu wanalala kwa milioni ngapi kwa usiku mmoja," alisema mwenyekiti huyo.

Mbowe alisema mapato yote yanayopatikana mbugani, yananufaishi wananchi wanaopakana na misitu hiyo ama hifadhi za wanyamapori.

Kuhusu umaskini wa watu wa Mang'ola, Eyasi na Karatu walionao, Mbowe alisema hakuna msingi au mfumo wowote ambao serikali imeweka kwa ajili ya kusaidia wakulima wa vitunguu wa Mang'ola vikabadilisha maisha yao.

Awali Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini anayemaliza muda wake, Godbless Lema, akizingumza na wananchi hao, alisema:

"Umaskini wa nchi hii haujasababishwa na Mungu, na hii biashara ya kwenda kanisani mnaukemea umaskini, Mungu anachukia. Umaskini haukemewi kwa jina la Yesu, umaskini unaondolewa kwa bidii, maarifa na kazi.

"Vitunguu vyote vinavyolimwa hapa bei inapangwa na Wakenya. Mahali ambako mnazalisha vitunguu vinavyokwenda dunia nzima. Vinakwenda Dubai, Abudhabi, Uarabuni, Bahrain, Oman, Kuwait.

"Karatu inazungukwa na mbuga za wanyama tatu; Manyara, Ngorongoro, Serengeti na jirani wapi hapa, Tarangire. Maana yake Karatu ndio mji wa kwanza kuwa katikati ya mbuga zote za wanyama.

"Ilitakiwa iwe na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa kama KIA. Wazungu watoke moja kwa moja Marekani wanatua hapa, wanakwenda mbugani kwa urahisi.

"Kama serikali ingezuia hoteli kujengwa ndani ya mbuga za wanyama za Ngorongoro, Serengeti, Manyara na Tarangire; hoteli zote zingejengwa ndani ya Mji wa Karatu, mngepokea wageni wengi hapa na umaskini huu usingekuwapo."

Hiyo ilikuwa siku ya kwanza ya siku 21 mfululizo za mikutano iliyotangazwa na CHADEMA kwa Kanda ya Kaskazini.

# INEC yataja sababu za kuahirisha maboresho Daftari la Wapigakura

**Na Adela Madyane,** KIGOMA

TUME Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) imeeleza sababu ya kuahirisha maboresho ya Daftari la Kudumu la Wapigakura hadi Julai 20 mwaka huu kuwa ni kuzingatia maoni ya wadau katika mikutano iliyofanyika Dar es Salaam na Kigoma.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini Kigoma, Mwenyekiti wa INEC, Jaji Jacobs Mwambegele alisema awali uzinduzi ulipangwa kufanyika Julai Mosi, mwaka huu na baada ya kusogezwa mbele, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa atazindua.

"Tume imezingatia maoni na ushauri wa wadau. Hivyo, zoezi la uboreshaji Daftari la Kudumu la Wapigakura litaanza tarehe 20 hadi 26 Julai, 2024 badala ya tarehe Mosi hadi 7 Julai, 2024, mkoani Kigoma na uzinduzi utafanyika siku hiyo ya tarehe 20 Julai, 2024," alisema.

Alifafanua kuwa tume ilifanya mikutano tisa ya wadau ngazi ya taifa mkoani Dar es Salaam kati ya Juni 7 hadi 15 mwaka huu na kwamba mkutano wa wadau ngazi ya Mkoa wa Kigoma ulifanyika Juni 19 mwaka huu.

Aliwataja wadau waliokutana na tume ni pamoja na viongozi wa vyama vya siasa, viongozi wa dini, wawakilishi wa asasi za kiraia, wahariri wa vyombo vya habari, waandishi wa habari, maofisa habari wa mikoa na halmashauri, wawakilishi wa makundi mbalimbali ya vijana, watu wenye ulemavu, wanawake na wazee wa kimila.

"Vyama vya siasa vilitoa maoni na ushauri wa kupatiwa muda wa kutosha kwa ajili ya kupata mawakala wa uandikishaji ili mawakala hao waweze kushiriki katika zoezi kikamilifu.

"Aidha, vyama vilishauri tume isogeze mbele muda wa kuanza kwa zoezi la uboreshaji ili kutoa fursa kwa wao kuhamasisha wananchi na wafuasi wao kujitokeza katika zoezi hilo," alisema Jaji Mwambegele.

Wengine ni taasisi na asasi zilizoomba kibali cha kutoa elimu ya mpigakura wakati wa uboreshaji ambazo zilieleza kuwa kibali kinapotolewa na tume huwa ni muda mfupi kufikia uboreshaji kuanza na wakashauri tume ione namna ya kutoa kibali kwa muda utakaowawezesha kupata fedha kutoka kwa wafadhili ili zoezi likianza nao waanze kutoa elimu hiyo.

Maoni mengine ya wadau yaliyosababisha tume kufikia uamuzi huo wa kusogeza mbele tarehe ya kuanza na kuzindua uboreshaji daftari ni yale ya kuishauri tume ijipe muda wa kutosha kutoa elimu ya mpigakura kwa wadau na wananchi kabla ya kuanza kwa zoezi lenyewe, ili wananchi wengi waelewe zoezi husika na hivyo kuwawezesha kujitokeza kwa wingi wakati litakapoanza.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hoja za waliokuwa wafanyakazi kiwanda cha UFI zifanyiwe kazi

**KIWANDA** cha Ubungo Farm Implements (UFI) cha Ubungo, Dar es Salaam kilichokuwa kinazalisha zana za kilimo kimebinafishwa, hivi sasa hakizalishi tena zana hizo, kinazalisha mabomba ya maji.

Ni hali inayokinzana na dhamira ya mwasisi wake, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere ambaye serikali yake ilikianzisha mwishoni mwa miaka ya 1960 kwa lengo la kuzalisha zana za kilimo ili wakulima wawe na uhakika wa kuzipata kwa urahisi nchini na kwa bei nafuu.

Kukiwa na mabadiliko hayo ya matumizi ya kiwanda, kwa miaka 26 baadhi ya waliokuwa wafanyakazi wa kiwanda cha UFI ambacho hivi sasa kinaitwa TSP, wanasotea haki zao.

Wanadai wameshaandika zaidi ya barua 40 kwa mamlaka mbalimbali nchini tangu mwaka 1998 bila mafanikio yoyote. Hadi kiwanda kinabinafisishwa mwaka 1998, kilikuwa na wafanyakazi 508 wanaodai stahiki zao za malipo ya mishahara, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na posho nyinginezo.

Taasisi ambazo wamekuwa wakielekeza barua zao kushughulikia madai yao ni pamoja na Bunge na Ikulu. Hata hivyo, wanadai hawajui tarehe ya kulipwa stahiki zao.

Kwa mujibu wa Katibu wa Kamati ya Ufuatiliaji Mafao ya Wafanyakazi wa Kiwanda cha UFI, Makamba Kigome, wanachodai ni kupunjwa katika malipo ya mtumishi na familia zao - kwamba hayakulipwa kulingana na umbali wa kila mmoja anakotoka, pia kutozingatiwa ngazi ya mshahara wa mtumishi.

Madai mengine ni posho ya kufungasha mizigo; haikuwafikia watumishi licha ya kuwapo kwenye mchanganuo wa malipo ya UFI.

Hoja zingine ni kutofuatwa Mkataba wa Hali Bora Sehemu ya Kazi, malimbikizo kulipwa kwa kutofuata mabadiliko ya mishahara tangu Julai 1994 hadi Julai 1998, kutolipwa malimbikizo ya likizo badala yake walilipwa likizo moja pekee ya mwaka 1994.

Wafanyakazi hao pia wanadai posho ya kujikimu kwa kipindi cha miezi mitatu wakati wanasubiri kulipwa mafao ya kuachishwa kazi. Barua zao zimeelekezwa kiwanda cha UFI wakati huo, Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC) na uliokuwa uongozi wa UFI.

Tunafahamu kuhusu barua yao ya Februari 14 mwaka huu waliyomwandikia Spika wa Bunge, Dk. Tulia Askon. Maudhui yake yanahusu wafanyakazi 271 wa kiwanda cha UFI, wanaoeleza kuwa baada ya mchakato wa ubinafsishaji, walilipwa sehemu ya malimbikizo ya mishahara ya miezi sita.

Wanadai hakuwalipwa mafao ya wafanyakazi licha ya kuwa wametimiza masharti ya kuwa kulipwa mafao, yaani walikuwa wametumikia kiwanda zaidi ya miezi 120 (kwa vigezo vya Mfuko wa Pensheni kwa Mashirika ya Umma (PPF) na NPF wakati huo.


Kimsingi, wafanyakazi wanada haki zao za msingi kwa kuwa walijiunga katika mifuko ya jamii ya PPF na NPF na wakachangia michango yao kutoka katika mishahara yao kwa mujibu wa sheria.

Ni vyema mamlaka husika zikamaliza suala hilo sasa kwa kuwa walishafikisha malalamiko yao sehemu mbalimbali, zikiwamo Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Fedha, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Ofisi ya Waziri Mkuu. Baadhi wamefariki dunia pasi na kulipwa stahiki zao.

Ofisi ya Spika ambayo wameshaiandikia, isadi kundi hili kupata stahiki zake kwa kuwa madai hayo ni ya muda mrefu ilhali wahusika wanalalama kuishi katika hali ngumu inayohatarisha maisha yao na familia zao.

Hoja za wafanyakazi hawa wa zamani wa kiwanda cha UFI zifanyiwe kazi na mamlaka husika za serikali ili kutenda haki kwa kundi hili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Uchaguzi unakuja, vijana wote msikubali kutumiwa na wanasiasa

Na Sabato Kasika

**VIJANA** ni nguvu kazi ya taifa, hivyo ndivyo iilivyo, ili nguvukazi hiyo iweze kuzaa matunda, ni muhimu vijana wenyewe wajitambue wajue wajibu wao na watumike kwa manufaa yao na ya umma.

Pamoja na kwamba wao ni nguvukazi ya taifa au taifa la kesho, bado wako baadhi yao ambao huwa wanatumiwa vibaya na wanasiasa hasa wakati wa kampeni za uchaguzi kwa kufanya vurugu au fujo.

Kimsingi, mwamko wa vijana unaendelea kukua kadri miaka inavyokwenda, hasa kutokana na hamasa zinazotokana na makundi mbalimbali yakiwamo ya wanasiasa na wanaharakati.

Ni zaidi ya miaka 30 sasa tangu vijana waanze kuhamasika kwenye siasa baada ya uchaguzi wa mwaka 1995 ambao baadhi yao walifukuzwa vyuoni baada ya kubainika kuwa wanashabikia siasa.

Lakini mwamko huo, kumekuwapo baadhi yao ambao kama nilivyoeleza awali kuwa hutumiwa na wanasiasa kwa manufaa ya hao wanaowatuma, kitendo ambacho ni wazi wanajiharibia mbele ya jamii.

Mwaka huu ni wa uchaguzi wa serikali za mitaa, ingekuwa ni vyema vijana wasikubali kutumika, badala yake wawe mstari wa mbele kuufanya uchaguzi huo kuwa wa amani na utulivu.

Isiwe kama ambavyo imewahi kutokea miaka ya nyuma kufuatia baadhi ya vijana kushiriki vurugu kwa kushambuliana na wenzao wa vyama vingine wakati wa kuelekea au kutoka kwenye kampeni.

Kuwapo kwa vurugu au fujo huku viongozi wao wakiwa kimya bila kukemea, ni wazi wanatumika vibaya. Hivyo ninadhani ni vyema sasa vijana kuamka na kujua haki na wajibu wao katika uchaguzi.

Miongoni mwa haki na wajibu ni kuchagua na kuchaguliwa, si kushiriki katika matukio ya kuharibu uchaguzi, kwa lengo la kunufaisha wale waliowatuma na kuwaneemesha, huku wao wakiibaki kama walivyo.

Ni haki yao kujiunga na vyama hasa kwa wale waliotumiza umri wa miaka 18, lakini kukubali kutumiwa na wanasiasa badala ya kuandaliwa kuwa viongozi wa baadaye, si sahihi.

Siasa, uongozi, na utawala ni mada ambazo zinaweza kuwa ngumu kuzungumza juu yake kwani zinahusisha masuala magumu ya kijamii, kiuchumi na kisiasa, hivyo ni muhimu kufanya siasa kwa umakini.

Ni muhimu kuelewa kuwa siasa, uongozi, na utawala vina uhusiano wa karibu. Siasa ni mchakato wa kuunda sera na maamuzi ambayo yanashughulikia masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Lakini pia, uongozi ni uwezo wa kushawishi watu kufuata maamuzi yako na kufanya kazi pamoja kufikia malengo fulani.

Utawala ni mchakato wa kutekeleza sera na maamuzi ambayo yamechukuliwa.

Ni vyema wanasiasa wakatumia njia hiyo ya kushawishi watu kufuata maamuzi yao ambayo ni sahihi kwa manufaa yao, jamii na taifa kwa ujumla, badala ya kushawishi kufanya vurugu au fujo.

Vilevile, ni vyema wanasiasa wajue kuwa siasa, uongozi, utawala na uwajibikaji ni mambo muhimu katika kuendesha jamii na taifa. kwa kusimamia na kuongoza masuala hayo kwa njia nzuri.

Njia hiyo nzuri ni kutoshirikisha vijana katika vurugu ili kupata uongozi, bali inawezekana kujenga na kuandaa vijana imara, ambao wanaandaliwa kuwa viongozi bora wa taifa la kesho.

Hivyo, ingekuwa ni vyema vyama vya siasa kuanza kuendelea kuwaandaa vijana wao ambao ninadhani kwamba wanaweza kuwa viongozi ili washiriki katika uchaguzi ujao.

Wasiwe watu wa kukubali kushiriki kwenye matendo ambayo si mema ndani ya jamii, kwani kuwashirikisha kwenye vurugu ni sawa na kuwandaa kuwa watu wasiofaa katika jamii.

# Mbunge apokewa kwa mabango msibani, mwenyewe aanika kiini

**Na Ambrose Wantaigwa**

MBUNGE wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara alipokewa kwa mabango na baadhi ya wananchi katika Kata ya Sirari, wakitaka aeleze alivyoshughulikia matibabu ya waathirika wa ajali iliyohusisha mashabiki wa mpira jimboni kwake.

Katika ajali hiyo, mkazi wa Sirari, Justin Mataro (28), alifariki dunia huku wengine 20 wakijeruhiwa wakati wakitoka kushuhudia mechi ya fainali za Kombe la Waitara lililodhaminiwa na mbunge huyo.

Tukio hilo la wananchi kubeba mabango lilitokea wakati mbunge huyo alipofika kuhani msiba nyumbani kwa shabiki huyo. Baadhi ya waombolezaji walijitokeza wakiwa wamebeba mabango yenye ujumbe unaoonesha kutoridhishwa na namna mbunge wao alivyoshiriki kufanikisha matibabu ya waathirika wa ajali hiyo.

Baadhi ya mabango hayo yalieleza familia ya marehemu kutopokea mchango wowote wa rambirambi kutoka kwa mwakilishi huyo wa wananchi bungeni.

Jeshi la Polisi lililazimika kuimarisha ulinzi, lakini halikutumia nguvu, maziko yakafanywa kwa mujibu wa ratiba iliyopangwa.

Mkuu wa Polisi Wilaya ya Kipolisi Sirari, Chausiku Masasi aliwaambia waombolezaji kwamba jeshi hilo linamsaka dereva wa gari aina ya Coaster lililohusika na ajali hiyo ambaye hata hivyo jina lake halikufahamika mara moja.

Alisema dereva huyo anasakwa kutoka na tuhuma zinazomkabili za kutenda makosa barabarani.

Alisema kila mtumiaji chombo cha usafiri anapaswa kutii sheria za barabara bila shuruti, huku akiwataka pia abiria kudhibiti madereva wanaowaona wakivunja sheria za barabarani kwa kutoa taarifa sahihi ili askari wa usalama barabarani wachukue hatua.

Mkuu wa Polisi alisema jeshi hilo linaendelea kufanya uchunguzi ili kujiridhisha iwapo kuna sheria yoyote ilivunjwa wakati wa mfululizo wa matukio hayo ili hatua sahihi ziweze kuchukuliwa dhidi ya wahusika.

Akizungumza katika maziko hayo, Mbunge Waitara aliwatuhumu baadhi ya wapinzani wake kisiasa (huku akiwataja kwa majina) kwamba wana lengo la kumchafua kwa kuwa ana malengo ya kutetea kiti chake cha ubunge.

"Na wale vijana waliotumika (kubeba mabango) wala siyo wa chama chetu, wamepewa pombe, wamekunywa na Sh. 5,000... unakuja kuwaambia wanafamilia eti msipokee rambirambi ya mbunge," alisema Waitara.

Msemaji wa Familia, Nyangi Robare alisema familia haikutuma mtu yeyote kuandaa mabango kwa ajili ya mbunge huyo huku




Kituo Kidogo cha Polisi Mwenge, Dar es Salaam kikiwa kimezungukwa na maji yatokanayo na mvua iliyonyesha mwanzoni mwa juma hili. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wataalamu wa afya 450 kutibu Arusha bila malipo

**Na Beatrice Shayo**

WATAALAMU wa afya 450 kutoka hospitali mbalimbali nchini na taasisi 40 wanatarajiwa kutoa matibabu na vipimo bila malipo kwa siku saba kwa wananchi wa Mkoa wa Arusha.

Mkuu wa Mkoa huo, Paul Makonda, alibainisha hayo jana kuwa baada ya kukagua maandalizi ya kliniki hiyo ya afya inayotarajiwa kuzinduliwa kesho kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid.

Alisema wataalamu hao, wakiwamo madakatari bingwa watatoa matitabu kwa wananchi bila gharama yoyote, hivyo ni muhimu wakajitokeza kwa wingi na kutibiwa.

"Ninaomba kuwakaribisha wananchi wote wa Arusha kujitokeza kwa wingi kwenye kliniki hiyo; matibabu na dawa vitatolewa bure kwa kila mwananchi atakayebainika na kugundulika kuwa na magonjwa ya aina yoyote.

"Ndugu zangu asiwaambie mtu, kwenye suala la afya kuna watu wameuza nyumba zao, kuna watu wameuza viwanja, kuna watu wamefilisika biashara zao katika kupambana kuuguza ndugu zao na kuna nyakati ndugu zetu wameshindwa hata kukomboa miili ya ndugu zao kutokana na madeni ya gharama za matibabu.

"Neema hii ambayo Mungu ametupa tukaitumie na mikono ya watumishi wa Mungu ikafungue baraka ili tukapate afya kupitia madaktari wetu hawa," alisema.

Makonda alizitaja hospitali na taasisi zitakazoshiriki kliniki hiyo na kutoa madaktari wake bingwa ni pamoja na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, Hospitali ya Kanda KCMC, Hospitali ya Kanda Benjamin Mkapa, Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI) na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Hospitali ya Mawenzi, SAIFEE na hospitali na taasisi zingine za ndani na nje ya Mkoa wa Arusha.

# Mageuzi uendeshaji miundombinu yafungua fursa tele soko la chakula

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Uchukuzi imesema mageuzi katika usimamizi na uendeshaji miundombinu ya uchukuzi yamefungua soko kubwa duniani kwa bidhaa za chakula.

Akizungumzia fursa hizo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Prof. Godius Kahyarara, alisema jana kuwa mazao hayo ni pamoja na matunda, mboga, nyama, samaki na rungis.

Katibu Mkuu alisema Ufaransa imekubali kufungamanisha fursa na maboresho ya miundombinu ya reli, bandari na viwanja vya ndege na kuitumia Tanzania kama kituo kikubwa cha kuzalisha mazao mbalimbali yanayoingia katika soko hilo.

Prof. Kahyarara alisema wawakilishi wa soko hilo na kampuni kubwa zilizo katika soko hilo wanatarajiwa kutembelea miundombinu hiyo mapema mwezi Julai mwaka huu.

Alisema wameahidi kufanya uwekezaji katika mafunzo ya kuandaa bidhaa za kuingia katika soko hilo, uwekezaji katika miundombinu ya mnyororo wa baridi (Cold Chain).

"Pamoja na uimarishaji uzalishaji wa nyama pamoja na samaki kwa ajili ya soko la nje, makubaliano yamefikiwa ambapo Mamlaka ya Biashara (TanTrade) itaandaa kongamano maalum la kuhamasisha uwekezaji na biashara kwa ajili ya soko hili kubwa kuliko yote katika nchi za Ulaya," alisema.

Kwa upande wa mageuzi yanayoendelea, Prof. Kahyarara alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameweka historia katika miundombinu barani Afrika kwa kuwa Rais wa kwanza kujenga mtandao mrefu wa reli kuliko nchi nyingine Afrika.

Alisema kwa sasa mtandao huo ndio wa kwanza kwa kuunganisha nchi za Tanzania, Burundi, DRC huku upande wa Uganda utaanza ujenzi wa reli mwaka huu na njia nyingine ni kupitia Ziwa Victoria.

Katibu Mkuu huyo alisema upande wa Uganda utakuwa fursa kutumia reli za Tanzania na kuunganisha kupitia meli maalum za kubeba mabehewa (Wagon Ferry).

Kuhusu bandari, Prof. Kahyarara alisema wamekamilika upanuzi wa njia ya kuingilia bandarini kutoka mita 140 mpaka mita 170 pamoja na kuchimba kina cha bandari mpaka kufikia mita 15.5.

"Hivi sasa wawekezaji wenye uzoefu wa kimataifa katika bandari wanajenga mfumo wa kuhudumia bidhaa zinazohitaji joto maalum eneo la Kurasini (Cold Chain) au Green Terminal ambayo itakuwa na miundombinu ya kisasa ya kuhifadhi ubora wa bidhaa kama matunda, mboga, samaki na nyama. Mfumo huo wa bandari umeunganishwa moja kwa moja na reli," alifafanua.

# HABARI PICHANI




Rais Samia Suluhu Hassan na mgeni wake Rais wa Guinea-Bissau, Umaro Embaló, wakishuhudia utiaji saini Mkataba wa Mwongozo wa Ushirikiano baina ya nchi mbili, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, akitia saini kwa upande wa Tanzania pamoja na Waziri wa Mambo ya Nje na Uhusiano wa Kimataifa na Jamii wa Jamhuri ya Guinea-Bissau, Carlos Pereira akitia saini kwa upande wa nchi yake. **PICHA IKULU**



Vyombo vya moto vikipita maji yaliyotuama katika Barabara ya Nyerere eneo la Vingunguti, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, akihutubia wananchi wa Kansay, Karatu, mkoani Arusha jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mwenyekiti wa Wamiliki wa Daladala Mkoa wa Dar es Salaam, Vatfad Kismat, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi na kuwataka wamiliki wote walipe kodi. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Wachuuzi wa machungwa katika Soko la Buguruni, jijini Dar es Salaam wakipanga bidhaa zao. Chungwa linauzwa kati ya Sh. 50 na 100. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# MAISHA

JUNI 23, 2024
Nipa

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 13


**Saspenda itakutoa**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Huisha nyumba yako uifurahie



**HARUSI**


Ukurasa 12




# Kuwa mrembo

Ukurasa 14

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA







| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| C | ■ | P | E | N | D | O |
| H | ■ | ■ | ■ | Y | ■ | N |
| O | ■ | P | A | O | ■ | D |
| C | H | A | ■ | K | O | O |
| H | ■ | N | O | A | ■ | S |
| E | ■ | G | ■ | ■ | ■ | H |
| A | G | A | N | A | ■ | A |

## AMSHA AKILI

CHORA KWA KUUNGANISHA NAMBA KUANZIA 1-48 ILI KUPATA MCHORO KAMILI




## TOA TOFAUTI 5



## FUMBO TOTO


| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | ■ | | | | | |
| | ■ | ■ | ■ | | ■ | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | | | ■ | | | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | ■ | | ■ | ■ | ■ | |
| | | | | | ■ | |

Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

NOA, ZEE, ANA, BEE, NDEGE, IMARA, ELEZA, BANDA, WATALII, ENDELEA

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Juma alikwenda shambani kumsaidia mama yake kulinda mpunga usishambuliwe na ndege.

Akiwa shambani alimuona mnyama aina ya kenge akikimbia kuelekea kwenye dimbwi la maji. Juma alishtuka na kuanza kulia.

**Juma:** Mama nimemuona mamba kaingia kwenye lile dimbwi la maji

**Mama:** Hapana yule sio mamba bali ni kenge

**Juma:** Kwani Mamba mdogo anaitwa Kenge?

**Mama:** Hapana ila ni wanyama wa jamii moja lakini wako tofauti kwa ukubwa.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mke simtaki lakini watoto wangu ninawachukua!

***KARIBU tena msomaji wangu tuendelee kudadavua vituko ndani ya ndoa zetu. Tayari nimechambua kwa kina dalili mbalimbali zinazoashiria ndoa kufuatiliwa na nguvu za giza.***

Msomaji wangu mmoja akaniandikia hivi: “Ndoa nyingi ni kweli hazina raha au zinavunjika kutokana na wanawake wengi kupenda ndoa bila kujua misingi yake. Msingi mmojawapo ni upendo wa dhati. Mtu analazimisha kuolewa na mtu asiyempenda ili eti aonekane kaolewa au mwanamume ana fedha, huku moyoni hampendi, akijipa tumaini atampenda taratibu.

Unaweza kushindana na kisichopendeka moyoni? Itafika kipindi ukimwona unatamani hata afe, japokuwa unazuga kumpenda. Mwanamume akigundua humpendi atapagawa na kutoka nje kwa sababu ndoa haina furaha. Jamani, oleweni na watu mnaowapenda (ninaomba namba yangu ya simu isichapishwe).”

Naam. Sasa sikia kituko hiki; Umempenda kwa dhati, ukasimama naye madhabahuni ukaahidi kuishi naye kwa shida na raha hadi kifo kiwatenganishe.

Lakini baada ya watoto wawili tu, mmoja anasoma chekechea na mdogo ananyonya, unaibuka eti humtaki mke, umemchoka. Ebo! Inaingia akilini hiyo?

Kipo kisa kimoja ambapo mume hivi karibuni wakati mke akiwa amesafiri, akafungasha nguo zake na kupeleka sanduku kwa ndugu wa mke kwa maelezo kwamba amemchoka mkewe na kwamba hataki arudi tena kwake.

Lakini kwa maelezo ya kina, wanandoa hawa wamekuwa na mtafaruku wa kitambo huku wakisuluhishwa mara kwa mara. Mume ndiye amekuwa akimshutumu mkewe kuhusu mambo fulani fulani lakini bila ushahidi.

Ndugu za mke kuona hivyo wakaitisha kikao na upande wa mume kujadili kulikoni. Mkewe na nduguze, akiwamo mzee wa hekima na busara, wakakutana na mume huyo na ndugu zake kusikiliza pande zote mbili kujua kuna nini.

Upande wa mke ukamwuliza bwana yule swali moja tu kwamba, “kwanini hamtaki mkeo?” Naye akasema amemchoka na kwamba anachotaka ni watoto wake!

Akaulizwa, “Kama anajua sheria za nchi, zinasemaje kuhusu watoto?” Akaambiwa watoto bado ni wadogo na mkewe analo jukumu la malezi yao kisheria. Baada ya mazungumzo na majadiliano ya kina, ikaamuliwa kuwa yule mtoto mkubwa ambaye alitakiwa aanze shule ndiye abaki kwa babake na yule mdogo anayenyonya aendelee kuwa na mama yake.

Hata mke alipodai baadhi ya mali zake mbali na nguo, mume alikataa kwa madai kuwa ni mali ya watoto. Ndoa zingine bwana, watu wanazililia lakini zingine ni machungu matupu. Ukiwa nje hatayajua lakini ukiingia ndani ya ndoa ndipo utaona rangi zote. Au siyo?

Mpenzi msomaji, nimeweka hapa kwa kifupi ili upate picha kidogo kisha utoe maoni yako. Mimi nikajiuliza, kama kweli amemchoka mke huyo, na ni mke wa ndoa, kwanini asimwache kwa talaka mahakamani?

Je, hiyo ni haki kumwadhibu mwenzako pasipo sababu zenye mashiko? Ningeelewa kama anao ushahidi kwa mfano, kamfumania, au amezaliwa mtoto ambaye siyo damu yake na kadhalika. Lakini kusema tu ‘nimekuchoka’ siafiki hata kidogo.

Zipo habari za uchunguzi zinazoonesha kuwa ingawa pale kikaoni bwana huyo alikana kuwa na mwanamke wa nje, inasemekana yupo na siku ya kikao alikuwa jirani anafuatilia mazungumzo. Kama habari hizi ni za kweli, basi mwanamume huyu kwa hakika alikuwa hampendi mkewe. Huo ndio ukweli.

Huu ni unyanyasaji uliofichika ambao jamii yafaa iutoe hadharani ili ndoa nyingi zinazovunjika kienyeji zipone. Kama kweli umemchoka mwenzako, na sababu za msingi unazo zikiambatana na vielelezo au ushahidi, mwache kwa mujibu wa taratibu na sheria za nchi.

Vinginevyo, mke huyo utakuwa umemfanyia ukatili kwa kumwacha kienyeji njiapanda pasipo sababu. Anastahili awe huru katika kuendeleza maisha yake mengine.

Hata hivyo, mke huyu akithibitisha kuwa mumewe anaye mwanamke mwingine anayemzuzua na kupata ushahidi, anaweza kufungua madai ya talaka mahakamani ili sheria iweze kutoa haki kwa pande zote za wanandoa hawa pamoja na watoto. Maisha Ndivyo Yaliyo.

Wanaume wengi wanaoacha wake zao kwa maelezo hayo juu wameishia majuto. Mpenzi msomaji, niachie hapa ili nawe uchangie kimbwanga hicho.

***Pia kama nawe unacho kisa, kituko kinachokuhusu au jirani au jamaa yako nitumie ujumbe mfupi kupitia simu ya kiganjani 0715268581 au pia WhatsApp kwa namba hii. Au Email: fwingia@gmail.com***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi

# Bado unatamani mapato ya aibu?

KILA kiongozi wa kiroho anapaswa kujiuliza “kwa nini ninamtumikia bwana?”

Amini usiamini kuna viongozi wengi ambao wamesahau wito wao na maana yake. Wameanza kufanya huduma kwa ajili ya mapato.

Ndio maana leo kupitia waraka wa Mtume Paulo kwa Timotheo, ninatamani na mimi kuwakumbusha, “Je, wanatamani fedha ya aibu?”

Ninaakumbuka mwanzoni mwa mwaka huu, hata Mkuu wa Jimbo la Kilimanjaro Kati la Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Mch. Javason Mrema, aliwanyooshea kidole baadhi ya wachungaji wanaojifungamanisha na aibu ya kuomba fedha kutoka kwa waumini wenye uwezo kiuchumi.

Alisema fedha ya aibu ni kuanzia ile mchungaji anaipata pasipo kufanya kazi au kutumia fedha nje ya utaratibu.

“Aibu nyingine ni kuomba fedha kwa washarika wenye uwezo kwa ajili ya matumizi yako binafsi na si kwa ajili ya usharika.

“...kwahiyo, mbali na kulichunga kundi la Bwana kwa moyo, na kwa upendo. Wachungaji jiepusheni na fedha na mapato ya aibu.

“Niwasihi sana wachungaji wenzangu pamoja na watumishi wote kwa ujumla, kuepuka sana fedha au mapato ya aibu.

“Sisi ni wachungaji na Bwana ametuita kuwa wachungaji... tuwe wapole, tusiwe wakali, tukemee dhambi kwa staha.

“Tunapaswa kuwa wanyenyekevu na kuwa kielelezo na mfano wa kuigwa na washarika na jamii kwa ujumla,” alisema.

Mchungaji huyo alikwenda mbali zaidi, akisema wachungaji wa sasa wanapaswa kuwa na tafakuri ya kina kuhusu utekelezaji wajibu wao wa kuchunga kondoo.

Kwamba kazi ya kuchunga kundoo kwa moyo, si nyepesi, hivyo mchungaji aliyepakwa mafuta, anapaswa kulichunga kundi lake kwa hiyari, na siyo kwa kulazimishwa.

“Niwakumbushe ndugu zangu wachungaji, kwamba mmepewa wajibu mkubwa na mzito wa kulichunga kundi la Bwana. Mmekabidhiwa kundi la Bwana katika sharika na mitaa kwa ajili ya kulichunga, kulisimamia na kuliongoza,” alisema.

Sambamba na kutambua wajibu huo wa kulichunga kundi kwa hiyari, Mkuu wa Jimbo alisisitiza kuwa pia wanapaswa kulichunga kwa moyo.

“Usifanye kwa kuwa kuna anayekusimamia, tulitunze kwa upendo ili waumini wajue kuwa mchungaji anatutunza kwa moyo lakini kwa upendo pia.

“Mbali na kulichunga kundi la Bwana kwa moyo na kwa upendo, wachungaji jiepusheni na fedha na mapato ya aibu,” alisisitiza.

Mkuu wa Jimbo pia alielekeza wachungaji na watumishi kushirikiana na kufanya kazi kwa bidii, ili familia zao ziishi maisha mazuri.

Zaidi aliongeza, “Tutumike kulichunga kundi lakini tusiwe wavivu, tufanye kazi kwa bidii kuimarisha hali zetu za kiuchumi katika familia zetu.”

Mimi sitamani hata siku moja kuja kuwaza kwa kutumia tumbo langu.

Naamini katika kuacha alama za kizalendo katika jamii yangu na taifa langu.

Jambo la pili. Nyie kina mama! unajisikiaje kuharibu nafsi za watoto wako na kubeba laana?

Waache watoto wakue wakimfahamu baba yao, kama baba yao, na siyo mtu katili. Hivi sasa ukizunguka mtaani kwako, utaona baadhi ya kinamama wako na watoto wao, wakiwa na makasiriko dhidi ya baba zao.

Wazazi wa kiume ukiwaona ni kama mabuldoza yanayotengeneza barabara inakuwa na lami nzuri, halafu ikishamaliza kazi, anayeliongoza anaambiwa hilo buldoza halitakiwi kupita tena kwenye hiyo barabara, itaharibu barabara.

Mara nyingine laana zinakuja kwenye familia kwa sababu ya mambo kama hayo.

Iko mifano hai huko mitaani tunakoishi, tunaona kuna familia watoto walikuwa juu na baadaye wamesambaratika, wakaisha kabisa!

Na jambo zuri zaidi ni kwamba, baba wala halaani, lakini Mungu pia ni wa haki. Kinamama wa aina hiyo wanaona sehemu ya kutua mizigo yao ni kwa watoto.

Unaua familia na kuondoa umoja wa familia na kusababisha baba kukosa uthamani. Kinamama wanaotoa fedha na kuwafutia aibu waume zao, ili wasionekane hawana kitu au wanaume suruali; hao ni wale wanawake wenye akili zao, wanaojua kesho ya watoto wao.

Ndugu yangu kwa haya yanayoendelea, mama kumjaza mwanawe sumu ili amchukie baba yake, kisa mgogoro wao wa uhusiano, amka ombea uzao wa kiume.

Kama una mume, mwombee mume wako sana. Kama una mtoto wa kiume, mwombee sana!

****Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

## HARUSI









Kumbukumbu iliyotukuka kwa Gloria Samson Paulo, wakati akifanyiwa sherehe ya kuagwa iliyofanyika ukumbi wa Cavilam Jijini Dodoma.

MITINDO



# Saspenda itakutoa

KUPENDEZA sio kuvaa vazi la suti pekee, bali kuna aina nyingine ya uvaaji lazima utokelezee, ninachosema hapa ni kwamba utaweza kupendeza kwa kuvaa mkanda pekee.

Saspenda ni mkanda wa mwili unao saidia suruali yako isishuke na kukufanya utoke mtanashati zaidi unapokwenda kazini au matembezi ya kawaida.

Ukivaa mkanda huu usivae mwingine kwenye suruali yako, tafuta suruali inayokuenea vizuri na ambayo haijakubana sana.


Hii mikanda ina mitindo tofauti, kuna aina nyingi za kukufanya uwe na machaguo tofauti.

Wanaopenda hii Saspenda wengi ni watu watanashati, wanaofuatilia mitindo ya mjini.

Unatakiwa kuwa mjanja katika kupangilia nguo, ni muhimu kuendana na rangi na sio kuchanganya rangi nyingi.

Kama unapenda kuvaa mavazi za kupooza mikanda ipo ya rangi zote, nyeupe na nyeusi zipo pia.

Kwa wapenzi wa nguo za mikono mifupi, pia mnaweza kujiunga na mtindo huu.





UREMBO



# Kuwa mrembo

KILA mtu ana namna yake ya kutafsiri dhana ya urembo kulingana na malezi na tamaduni za mahali husika.

Wapo wanaoamini kuwa mrembo ni lazima awe na ngozi nyeupe, wengine hudhani kuwa ili kuonekana mrembo, lazima uwe na nywele ndefu, lakini pia wapo wanaodhani kwamba ili uwe mrembo ni lazima uwe na umbo namba nane, na wapo wanaojua urembo ni kuwa mwembamba au kuwa mrefu.

Dhana hii ni tofauti na wataalam wa afya ambao wanatafsiri urembo ni kuwa na afya bora katika maeneo kadhaa yafuatayo.

**SAFISHA NGOZI**

Hakikisha ngozi yako inakuwa safi muda wote. Unaweza kutumia njia mbalimbali kama vile kuondoa ngozi zilizokufa mara kwa mara.

Kuondoa mafuta yaliyoganda katika ngozi kwa kufanyia masaji ngozi yako ili kurahisisha mzunguko wa damu yako.

**SAFISHA NYWELE**

Tumia bidhaa za nywele, ambazo zinaendana na nywele zako na hakikisha unazingatia mambo muhimu katika uboreshaji wa nywele zako.

Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na kutokutumia vifaa vinavyounguza nywele.

**EPUKA VIPODOZI**


Tumia vipodozi pale inapobidi, usipendelee kutumia vipodozi mara kwa mara kwa sababu wakati mwingine matumizi ya mara kwa mara ya vipodozi, husababisha madhara katika ngozi yako, hasa unapotumia bila kufuata maelekezo ya wataalamu.

**SAFISHA MENO**

Usafi wa meno pia ni miongoni mwa mambo ya kuzingatia unapoamua kuboresha urembo wako. Hakikisha unapiga mswaki walau mara mbili kwa siku kila siku au kila baada ya kula.

Haya yameorodheshwa na wataalamu mbalimbali kuwa ni mambo yanayochangia urembo wa asili na mvuto wa ngozi na mwili.





MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Saladi ya matunda

SALADI ni mchanganyiko wa matunda mbalimbali au mboga zinazoliwa ambazo huandaliwa bila kupikwa.

Aina hii ya chakula wakati mwingine huitwa kachumbari ya matunda au mboga.

Unaweza kuandaa saladi hii kulingana na matamanio yako, uhitaji wa mlaji, bajeti yako au upatikanaji wa matunda.

**Mahitaji**

Nanasi moja kubwa, embe mbili kubwa, tikitimaji moja dogo, papai moja dogo, machungwa mawili madogo, ndizi tatu kubwa, kokomanga moja dogo na matunda damu matatu.

Aidha, zabibu mkungu mmoja, sukari vijiko vitano, maji ya moto nusu jagi, pilipili manga vijiko viwili vidogo, mayonise (kama utahitaji au unapenda) vijiko viwili vidogo.

**Maandalizi**

Osha matunda yote kwa maji ya uvuguvu ili kuua vijidudu vya maradhi.

Yakaushe na yamenye na kuyaweka kwenye vyombo visafi (angalau vilivyosafishwa na maji ya uvuguvu na kukaushwa).



Chemsha maji kisha changanya sukari na pilipili manga (yaache yapowe), kata matunda katika vipande vidogo vidogo, weka kwenye bakuli na kisha changanya, chukua mchanganyiko wako wa maji, sukari na pilipili manga kisha changanya kwenye matunda

Changanya mchanganyiko wako kisha tayarisha kwa ajili ya kula.

MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

# Tumia vyombo vya mbao pekee



WIKI mbili zilizopita, msomaji wangu kutoka Musoma alinitumia meseji kutaka kujua ubunifu wa matumizi ya mbao umeweza kutatua vifaa vyote vya jikoni.

Alinipa changamoto ya kupekua mtandaoni na maeneo yanayouza kazi za sanaa ili kujiridhisha kama kazi za wasanii wa kuchonga zimeongeza ubunifu, kutoka kwenye miiko, vibao vya kukunia nazi na vinu, hadi kutengeneza vifaa vyote vya jikoni.

Katika eneo wanakouza vifaa vya uchongaji Kariakoo, ubunifu umeleta masinia, bakuli, glasi, vijiko vikubwa na vidogo, visu vya kulia chakula, vikopo vya kuwekea chumvi, sukari na viungo mezani, pamoja na vifaa vya siku zote vnu, miiko na kibao cha kukuzia nazi.

"Sasa hivi unaweza kuamua nyumba yako ukatumia vifaa vya mbao kasoro tu sufuria na vingine vichache sana kama visu vya kukatia na chujio la kuopolea maandazi kwenye mafuta," anaeleza Mariamu Athanas, anayeuza aina hiyo ya vyombo.

Anafafanua: "Kwa wapenzi wa mbao, hakuna ambacho hawawezi kuchonga hapa nchini. Hata kama hakipo sokoni, ukienda na picha kwa wachongaji, unakipata kama kilivyo."

Hata hivyo, muuzaji wa vyombo vya udongo katika soko la Kariakoo, Khadija Ramadhan, anasema kwa wasiopenda vyombo vya mbao, wanaweza kujipatia vyombo vya rangi wazipendazo kwa kuwa vipo vya maumbo na rangi tofauti.

"Ukitaka rangi yoyote ya chombo, unaipata kama unavyoona kwenye nguo na rangi za nyumba. Kile unachotaka kikufurahishe ukiwa jikoni au kwenye meza ya chakula kwenye vyombo kipo," anasema.





# Huisha nyumba yako uifurahie



WENGI wetu tunapenda ndani ya nyumba zetu kuwe na mvuto wa kuridhisha nafsi zetu.

Pamoja na kupenda huko, tumekuwa tukishindwa kuziridhisha nafsi hasa kutokana na kukosa kipato cha kutuwezesha kutengeneza nyumba zetu kama nafsi inavyopenda.

Mtaalamu wa masuala ya ujenzi, Lucas Kwambikwa anasema zipo njia mbalimbali za kufikia angalau kwa kiwango fulani ambacho kinaweza kuridhisha nafsi kwa kuboresha nyumba yako ikawa na mvuto bila kutumia gharama kubwa.

Lucas anasema endapo nyumba yako imechakaa na haufurahishwi na mwonekano wake, unaweza kufumua rangi yake na kupaka upya na inaweza kuwa ileile au ukabadilisha nyingine, mradi uwe umeridhika nayo ili kuipa mwonekano mpya.

Anasema kubadilisha samani za ndani nako kunachangia kuipa mwonekano mpya nyumba yako, unaweza kufanya ukarabati mdogo ikiwamo kubadili kitambaa.

Mbali na samani, mapambo nayo yatakupa mwonekano mpya, kama uliweka yana muda mrefu yamechakaa, weka mengine mapya.

Anasema ni muhimu kuwa na picha yako kichwani ya namna unavyotamani kubadili nyumba yako ili kila unachofanyia marekebisho kiendane na matakwa yako.

Lucas anashauri kuondoa ndani ya nyumba vitu ambayo havitumiki ili kuacha nyumba kuwa na hewa ya kutosha na kukupa kufurahia kukaa muda mwingi bila kuchoka.


"Kwa mfano badala ya kuweka vitu vingi ukutani, ukatafuta picha moja kubwa ya mvuto na kuibandika, hiyo haitamchosha mtu kuitazama."

Anashauri kuepuka kununua vitu vingi na kuviweka ndani ya nyumba kabla ya kufahamu matumizi yake. Ni vyema kuhakikisha kila kitu kinachowekwa ndani ni kile kinachotumika.

Anataja baadhi ya vitu vingine vya msingi vya kuzingatia unapohuisha mwonekamo wa nyumba yako ni pamoja na pazia au zuria. Kwamba wakati wa kuviweka ni muhimu kuhakikisha rangi zake ni zile zinazoshabihiana na vitu vilivyomo ndani ya nyumba.

"Nyumba ni ubunifu, ukizingatia hili utafurahia nyumba yako na utapenda kukaa humo bila kuchoka."

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
BARUA YA UCHUMBA NATUMA 'BILIONI MOJA' PIA NAONGEZA MILIONI MIA TANO YAKUSOMEA BARUA...NASUBIRI JIBU LA MAHALI YA MKE
MUDA WA KUDHALILIKA KWA WAGANGA USHAFIKA!
JUKWAANI
UNATAKA HESHIMA KWA MKEO MIFUKO IMETOBOKA!
KWANI 'SH'KAMOO' SHILINGI NGAPI?
ANAKUJA ANDAA KANIKI
GARI LA MSHAHARA
NAFIKIRIA SIKU IKITOKEA NIMEMWAGWA NISIRUDI TENA MJENGONI
WEWE HUNA STAHAMALA UTAZIMA KAMA KIBATARI!
SINA TOTO BAYA KA'WEWE!
'ZE' SEM' TUMII'
NIMETAFUTA SIFA KWA WAPIGA KURA NIMEKULA NAO MIGUU YA KUKU NASIKILIZIA!
HII TV MBONA 'INACHENGA?"
LETE UNGO

## HABARI KIMATAIFA

# Gaza yaendelea kushambuliwa

**GAZA,** PALESTINA

SHIRIKA la kimataifa la Msalaba Mwekundu, limeripoti watu 22 wameuawa katika shambulizi la makombora lililolenga jengo la ofisi zake katika mji wa Gaza.

Shambulizi hilo lilifanyika usiku wa Jumamosi lilifanywa na ndege za kijeshi za Israel.

Ripoti zinaeleza kuwa jeshi la Israel limezidisha mashambulizi yake katika eneo lote la Palestina ambalo limezingirwa.

Wakati huo huo, kumeripotiwa majibizano ya risasi katika mpaka wa Lebanon kati ya wanajeshi wa Israel na kundi la wanamgambo linaloungwa mkono na Iran la Hezbollah, yameongezeka katika wiki za hivi karibuni na kuibua wasiwasi wa kuwa vita kamili.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, alisema juzi kuwa uhasama huo wa mpakani haupaswi kuigeuza Lebanon kuwa Gaza nyingine na alionya juu ya kuzuka kwa janga lingine la kibinadamu.

Licha ya onyo hilo, Israel inaendelea kushambulia Ukanda wa Gaza, huku hospitali mjini humo ikiripoti vifo vya watu 30.

Katika hatua nyingine, Qatar imesema inaendelea na juhudi za upatanishi kati ya Israel na kundi la Hamas kwa lengo la kufikiwa makubaliano ya usitishaji vita na kuachiliwa kwa mateka wa Israel.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Qatar, Mohammed bin Abdulrahman bin Jassim Al Thani, alizungumza hayo akiwa kwenye ziara nchini Hispania jana.

Akiwa na waziri mwenzake wa Hispania, Jose Manuel Albares, alisema wameafikiana kikamilifu kwamba amani ya haki na ya kudumu inaweza kupatikana ikiwa kutakuwepo suluhisho la mataifa mawili na kupatikana kwa taifa halisi la Palestina.

"Kwa hiyo tunapigia upatu kufanyika kwa mkutano wa amani utakaozijumuisha pande zote mbili pamoja na jumuiya ya kimataifa." Alisema Albares.

Qatar, Marekani na Misri, zimekuwa katika mazungumzo ya upatanishi kwa miezi kadhaa, lakini hadi sasa walifanikiwa kupata usitishwaji mapigano wa siku saba pekee mwezi Novemba mwaka jana, ambayo yaliwezesha kuachiliwa kwa mateka zaidi ya 100.

**DW**



Wafanyakazi wa mitambo ya kuzalisha umeme nchini Ukraine, wakikagua vifusi vya kituo cha usambazaji umeme kilichoharibiwa na makombora ya Russia katika viunga vya mji wa Kharkiv juzi. **PICHA: AFP**

# Viongozi Argentina, Hispania wavutana

**MADRID,** HISOANIA

RAIS wa Argentina Javier Milei, amerudia mashambulizi ya maneno dhidi ya Waziri Mkuu wa Hispania, Pedro Sanchez, akisema anaipeleka nchi katika maangamizi.

Akizungumza wakati wa ziara yake nchini humo iliyolenga kupokea tuzo iliyotolewa na taasisi moja ya mrengo wa kulia, alikemea siasa ya ujamaa inaozalisha umaskini unaotokana na wivu, chuki, na kutendewa kinyume cha sharia.

Pia alikosoa mipango ya serikali ya Sanchez ambaye pia ni mwanauchumi, huku akiwaonya Wahispania kuhusu hatari inayowakabili siku za usoni.

Ziara ya mwisho ya Milei nchini Uhispania ambayo aliifanya mwezi uliopita, ilibua mgogoro wa kidiplomasia ulioshuhudia nchi hiyo kumuondoa balozi wa Argentina nchini humo. Milei alikwenda katika jiji la Madrid kupokea tuzo iliyotolewa na taasisi ya Juan de Mariana kutokana na utetezi wake wa kuigwa wa mawazo ya uhuru.

**DW**

# Libya yakanusha kuhusika vita Sudan

**BENGHAZ,** LIBYA

SERIKALI ya Libya inayotawala eneo la mashariki, ambayo haitambuliwi na jumuiya ya kimataifa, imekanusha kuhusika katika vita vinavyoendelea nchini Sudan.

Kiongozi wa serikali hiyo, Khalifa Haftar anatumiwa kuwa karibu na kukipatia silaha kikosi cha RSF ambacho kinapigana na jeshi la Sudan.

Katika hotuba aliyoitoa Jumatano ya wiki hii katika Baraza la Usalama la Umoja wa Maraifa, mwakilishi wa Sudani Al Hareth Idriss, alithibitisha kwamba jeshi la Sudan lina ushahidi wa kuhusika kwa nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) kutuma silaha na risasi kwa RSF katika mkoa wa Darfur, kupitia Chadi, Libya na Jamhuri ya Afrika ya Kati.

Katika taarifa yake, serikali hiyo ilishangazwa kwa madai hayo na kukana kuhusika kwa namna yoyote vita vinavyoendelea nchini Sudan.

Ilizilaumu pande hizo mbili zinazopigana kwa kufanya uhalifu unaolingana na mauaji ya kikabila.

Kwa mujibu taarifa hiyo kwa vyombo vya habari, mwakilishi wa Sudan katika Umoja wa Mataifa anajaribu, kwenda njia tofauti kwa kuangalia mbali na kile kinachotokea nchini mwake.

Iliongeza taarifa hiyo kuwa shutuma hizo ni makosa na sio haki na kwamba Jeshi la Kitaifa la Libya linashutumiwa kimakosa.

"Libya haiingilii mambo ya ndani ya Sudan", ilisema taarifa hiyo.

Suala la uhusiano kati ya kiongozi wa Libya mashariki, Marshal Haftar na FSR inayoongozwa na Mohamed Hamdan Daglo limekuwa mjadala tangu kuanza kwa vita nchini Sudan.

Majenerali hao wawili wanasaidiana na kuimarisha uhusiano wao nan chi za Russia na Umoja wa Falme za Kiarabu.

**RFI**

# Kampeni za uchaguzi zaanza rasmi Rwanda

**KIGALI,** RWANDA

KAMPENI za uchaguzi mkuu nchini Rwanda zimefunguliwa rasmi, huku Rais Paul Kagame akionekana kukosa mshindani mwenye nguvu katika kutetea nafasi yake.

Zoezi la upigaji kura limepangwa kufanyika Julai 15 Julai, wapigakura watatakiwa kuchagua rais, wabunge na madiwani.

Kuna wagombea watatu katika nafasi ya urais, akiwemo Kagame, Frank Habineza, na Phillipe Mpayimana.

Watu milioni tano wamesajiliwa katika daftari la wapiga kura.

Kwa mujibu wa tume ya uchaguzi nchini humo, wagombea 500 wameidhinishwa kuwania viti 30 vya ubunge.

Katika wiki tatu zijazo, wanasiasa hao watapigana vikumbo katika maeneo mbalimbali nchini humo kutafuta uungwaji mkono kutoka kwa wapigakura.

Rais Kagame ambaye amekuwa madarakani kwa miongo miwili, anataka kuwania kiti hicho kwa awamu ya nne. Licha ya kupongezwa kwa kuleta amani nchini humo, anashutumiwa kwa madai ya kukandamiza upinzani, madai ambayo amekana.

**BBC**

SAFU

MAKALA

# RAIS SAMIA, HOJA YA KUFUTA ADHABU YA KIFO NCHINI INA MASHIKO, LAKINI...



Na Magabilo Masambu

Ni mwishoni mwa mwezi uliopita tu, tulisikia habari za kuuawa mtoto Asimwe Novart mwenye umri wa miaka miwili na nusu, aliyechukuliwa mikononi mwa mama yake katia Kijiji cha Bulamula, wilayani Muleba, mkoani Kagera.

TUME ya Haki Jinai iliyoundwa na Rais Samia Suluhu Hassan mwaka jana, imekabidhi ripoti yake.

Inaeleza kwamba Tanzania mpaka mwaka jana ilikuwa imetimiza miaka 28 bila kutekeleza adhabu ya kifo kwa wafungwa waliohukumiwa kunyongwa. Hadi Mei 2023, wafungwa waliohukumiwa kunyongwa hadi kufa walikuwa 691 nchini.

Tume hiyo pamoja na mambo mengine, inapendekeza Sheria ya Kanuni za Adhabu (Penal Code), Sura ya 16, ifanyiwe marekebisho ili adhabu ya kifo isiwe adhabu pekee kwa kosa la mauaji na kwamba adhabu hiyo sasa iwe ni kifungo cha maisha.

Wakati wa ukusanyaji maoni kuhusu adhabu ya kifo iendelee au ifutwe, yalitolewa maoni mchanganyiko; wapo waliopendekeza ifutwe na wako waliosema ibaki palepale na mimi nikubaliane na hawa wa kundi la pili waliyopendekeza adhabu ya kifo kubakia kama ilivyo na ikiwezekana badala ya kuwanyonga gizani sasa wanyongwe hadharani.

Ni kweli kwamba adhabu ya kifo hutumika kama adhabu pekee kuwahukumu wauaji haikuwa sawa, lakini kuifuta na mbadala wake kuwa kifungo cha maisha ninafikiri si sawa! Hii ni kwa sababu, dhamira na mazingira ya mauaji yanatofautiana.

Kuna hawa wanaoua ndugu zetu wenye ualbino na makundi mengine katika jamii kwa lengo la kupata viungo vyao eti kwa nia ya kupata utajiri.

Ni mwishoni mwa mwezi uliopita tu, tulisikia habari za kuuawa mtoto Asimwe Novart mwenye umri wa miaka miwili na nusu, aliyechukuliwa mikononi mwa mama yake katia Kijiji cha Bulamula, wilayani Muleba, mkoani Kagera.

Mazingira ya tukio hili - kuporwa na watu kutoka kwa mama yake, yanaonesha ukatili usiovumilika katika jamii.

Tunaweza kuona ni ukatili wa kiwango gani.

Sisi tulio na watoto wadogo tunaweza kujua ni maumivu kiasi gani aliyobaki nayo mama yake.

Hakuna jambo zito na lenye maumivu kama kumpoteza mtoto mwenye umri huo - miaka miwili na nusu, ni kipindi ambacho mapenzi kati ya mzazi na mtoto yanakuwa ni makubwa kuliko kipindi chochote.

Mheshimiwa Rais na Watanzania wote, wakati unasoma makala hii, jaribu kusikiliza sauti ya mtoto au watoto wako au wajukuu wenye umri kama wa Asimwe moyoni mwako wakikuita "babaa", "mamaa" au "bibii..."

Ni maumivu kiasi gani unayoyasikia kama ndiyo wangelikuwa wametendwa unyama kama aliyotendewa Asimwe?

Hata hivyo, katika mazingira kama haya, yanatolewa maoni kwamba sheria ya kunyongwa ifutwe kwa sababu inavunja haki za binadamu!

Kwahiyo, aliyeua katika mazingira haya, akaishi gerezani maisha yake yote huku akila kodi zetu bure ilhali amekatisha uhai wa Asimwe? Je, kumnyonga mtu wa aina hii ni kuvunja haki zaidi kuliko alivyotenda dhidi ya Asimwe? Huku ndiko kutekeleza haki za binadamu?

Katika taarifa iliyotolewa na Jeshi la Polisi inaeleza kwamba, baada ya msako mkali kushirikiana na raia wema, lilikamata watuhumiwa tisa wakiwa na viungo vinavyodhaniwa kuwa vya mtoto Asimwe, wakitafuta mteja.

Kama kweli ikithibitika kwa Mkemia kwamba ni vya Asimwe au ni vya mwingine, watu hawa wote walioshiriki kufanya kitendo hicho, wanapaswa kunyongwa mpaka kufa ili liwe fundisho.

Mauaji ya aina hii ni wazi yalipangwa kwa muda mrefu. Hivi sasa kunaripotiwa matukio mengine ya ukatili. Mbaya zaidi yanahusisha hadi kundi tulililoamini - walimu, viongozi wa dini na wazazi! Tukimbilie wapi?

Miaka kadhaa ijayo litakuwa taifa la namna gani hili? Nikuombe Mheshikiwa Rais na Watanzania wote tukubaliane adhabu ya kifo isitumike kama adhabu pekee kwa wauaji kutokana na sababu nilizozieleza hapo juu, lakini katika mazingira ya mauaji kama ya Asimwe, adhabu hiyo tukubaliane tu itekelezwe ili kulinda utu na heshima ya wenzetu, kama binadamu wanaostahili kupata haki ya kuishi kama wengine kwa mujibu wa Ibara ya 14 ya Katiba ya nchi yetu.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Dar es salaam-Tanzania**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Harusi imevunjika, jamaa anadai apewe mahari yake*



Na Adam Fungamwango

Hata hili nalo, wanamuziki wa dansi hawakuliacha nyuma. Walishawahi kulizungumzia. Mambo haya yalianza zamani sana. Marehemu Shaaban Dede akiwa na bendi ya Bima Lee, alitunga kibao kiitwacho, 'Shangwe ya Harusi' kinachofanana na kisa hiki.

DUNIANI kuna mambo ambayo mengine huwezi kuamini kama kweli yanaweza kutokea. Fikiria watu wanaahidiana kuoana, lakini siku ya ndoa bi harusi, au bwana harusi haonekani. Haji kabisa, au anatoweka muda mfupi tu kabla ya ndoa kufungwa.

Unaanza kuwa na maswali mengi ya kujiuliza, je mmoja alilazimishwa? Kuna nini nyuma ya pazia ya tukio hili, unashindwa kulipata.

Hebu niwape tu tukio moja la jamaa aliyekwenda kuoa. Akakusanya ndugu na jamaa zake kwenda ukweni. Kufika huko alikuta sherehe babu kubwa ikimsubiri. Lakini ilipofika muda wa kufungishwa ndoa, bi harusi hakuonekana.

Tafuta, tafuta na wewe. Mabibi waliokuwa naye walidai kuwa alikuwepo ndani muda wote, na asubuhi alikwenda saluni kupambwa kwa ajili ya ndoa. Dakika za mwisho aliwaaga kuwa anakwenda msalani, lakini hakurejea.

Hakuna chochote kilichoendelea. Harusi ndiyo ilikuwa imeishia hapo. Yaani imevunjika. Kililiwa chakula kilichokuwa kwa ajili ya sherehe hiyo, lakini tukio lililokusudiwa halikufanyika. Bwana harusi akarejea nyumbani na ndugu zake, jamaa na marafiki kwa majonzi.

Binti hakuonekana mpaka baada ya miezi sita, akarejea kwao. Tatizo lilikuwa nini? Mbona alijiandaa kwa kuolewa.

Kilichokuja kugunduliwa chini ya pazia, yeye mwenyewe akielekea alidai kabla ya bwana harusi huyo alikuwa na mwanaume mwingine. Hata hivyo hakuwa na uwezo, pia hakuwa na mpango wa kumuoa. Ilipotokea bahati ya kuolewa na huyo aliyetaka kumuoa aliachana naye.

Wakati siku hiyo yupo kwenye maandalizi ya kuolewa, akiwa saluni alipigiwa simu na mpenzi wake huyo wa zamani, akimwambia amepata pesa nyingi sana, hivi sasa anaweza kufanya chochote, na anaweza kumuoa pia.

Akamwambia kama ana mpango wa kuolewa asitishe haraka sana na aje kwake, kwani anataka kumfanya awe malkia. Binti alipomtaka amthibitishie kama maisha yake yamebadilika, akaingiziwa kiasi cha Sh. 500,000 papo hapo, akaahidiwa Sh. Milioni mbili kama akifanikiwa kutoroka kwenda kwake. Ndiyo maana akatoroka siku ya harusi.

Alipofika alikuta ni kweli, maisha ya mpenzi wake huyo yamebadilika sana, na alichoahidiwa alikipata. Miezi michache ya furaha yao ilikatishwa na jamaa kukamatwa na askari kwa kile kilichodaiwa wizi wa mali ya kampuni aliyokuwa akifanyia kazi. Biashara ikaishia hapo, binti akarejea nyumbani kwao, pamoja na juhudi zote za kutaka arudi amuoe japo bila sherehe tena, ilishindikana. Jamaa akakataa katakata kutokana na aibu aliyoipata mwanzo. Hapa tunaona kuwa kumbe likitokea jambo kama hili la harusi kuvunjika, bwana au bibi harusi kutoweka kabla ya ndoa kuna sababu nyuma ya pazia kama hii, au inayofanana na hii.

Hata hili nalo, wanamuziki wa dansi hawakuliacha nyuma. Walishawahi kulizungumzia. Mambo haya yalianza zamani sana. Marehemu Shaaban Dede akiwa na bendi ya Bima Lee, alitunga kibao kiitwacho, 'Shangwe ya Harusi' kinachofanana na kisa hiki.

"Penzi limegauka majozi, niliyetaka muoa, kanisaliti, niliyetaka muona kanisalini jamani shangwe na harusi imekuwa kitendawili.

Kinamama aliokuwa chumba kwa bi harusi, wakiimba kwa shangwe, wakijimwayamwaya, kwa furaha, kupokea mume. Bomu la simanzi limepasuka hadharani, nilipoingia ndani, nisimkute Salma, tausi wangu miye, katoweka.

Shangwe ya harusi imekuwa kitendawili, kilichokosa mfumbuzi, jamani eee."

Baada ya tukio hilo, wazazi nao wanaonyesha kufedheheshwa na binti yao, nao wakasema.

"Uso wangu mimi nitauweka wapi, aibu mama, amenipa mwanangu, uso wangu Dede, nitauweka wapi, abu Momba, amenipa mwangu, kama ni mchumba wa kulazimishwa vile, lakini kumbe alikubali mwenyewe."

Tukitoka kwa Bima Lee, marehemu Mbaraka Mwinshehe, yeye alitunga wimbo alioupa jina, 'Harusi Imevunjika', ikiwa na mashairi yafuatayo.

"Kweli nimepata niliyoyasikia, sikudanganywa ooo, kumbe uko Gabon, umeshaolewa na mtu mwingine.

Nasema nasikitika kwani ulichokifanya ni cha dhuluma ooo, wazimu si wazimu huku nimebaki nalia moyoni.

Sasa ufanye hima uwatumie barua wazazi wako oo, warudishe mahari yangu ili nipate tafuta mchumba mwingine."

Hapa jamaa anawasiliana na mchumba wake walioahidiana kuoana. Kila kitu kimeshapangwa hadi mahari imeshalipwa. Baadaye akasikia yupo nchini Gabon na ameshaolewa na mtu mwingine.

Baada ya kuongea na binti, sasa jamaa anawaambia jamaa zake kuwa harusi aliyotaka kuifanya imevunjika.

"Nawaarifu ndugu zangu wote, harusi imevujika jama. Niliyetaka kumuona, amenikatalia bila kosa mwenzenu."

Haya ndiyo maswahiba yanayowapata watu katika sayari hii. Dunia hii ina maajabu, utayaona mengi, utasikia mengim, utayapata mengi, yatakukuta mengi.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

KIJANA Heri alikutana na msichana Nuru katika duka fulani maeneo ya Chanika, Dar es Salaam. Baada ya kuongea waliyoongea wakakubaliana kuonana siku ya Jumapili kwenye nyumba ambayo alimuelekeza aje kuulizia. Siku ilifika kama walivyoahidiana, masaa machache kabla ya kuwasili Heri alianza kusikia harufu mbaya chumbani kwake, ambayo kwa uzoefu wake aligundua ni ya panya aliyekufa. Akafanya kila kitu ambacho alidhani kinaweza kumaliza tatizo kwani muda ulivyozidi kusonga mbele ndiyo harufu nayo ilizidi. Muda wa Nuru kufika ulikaribia. Njia mbadala aliyotumia kuondoa harufu ndiyo iliyoleta balaa zaidi.

# Harufu ya Panya-13

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

NILITESWA mimi. Napewa kazi si saizi yangu, wakati mwingine nashindishwa na njaa wakati chakula nimekipika mwenyewe. Nilikuwa naogopa kumwambia baba anaporejea. Niliteseka sana kusema kweli.” “Pole sana.” Mzee Raia alisema huku akitikisa kichwa. Heri hakusema lolote. Ilionekana kama yanayosemwa yamemuingia hadi amejisahau.

“Tulipokuwa wasichana wakubwa sasa, watu wengi walikuja kutaka kunioa. Hawakuwa wakimkuta baba. Walimkuta mama. Kuna waliokuja tu kuahidi kwa mdomo, wengine walileta barua kabisa, lakini mama alikuwa azichanachana na kuwarudishia pesa zao.

Watoto wake hakupata bahati hiyo kwa sababu walikuwa jeuri, hawana kauli nzuri kwa watu.

Wavivu, hata kupika hawajui. Sifa zote zilikuja kwangu mimi, kwa sababu mwanzo waliona kama wananitesa, lakini nilijua kumbe walikuwa wananipa mafunzo mazuri kwa maisha yangu ya baadaye.

Kila mtu alikuwa ananisifia siyu uzuri tu, tabia, kujituma kwenye kazi, hata mapishi.”

“Basi leo hapa huondoki bila kutupikia.” Heri akadakiwa kwa mara ya kwanza tangu Nuru alipoanza kutoa historia yake na kusababisha wenzake waangue vicheko.

“Kanunue mahitaji tu baba, utaomba kila siku niwe hapa, au nisiondoke kabisa.” Akajibu Nuru na kufanya vicheko viongezeke. “Enhee, lete habari.” Mzee Raia alimhimiza kuendelea.

“Basi, yule mama wa kambo baada ya kuona mabinti zake hawapati bahati ya kuuliziwa kuchumbiwa, alizidi kunichukia, maneno mama, nasikia ndiyo akaenda kwa watu wabaya sijui wachawi, nikatupiwa jini.

Niwaambie tu kubwa ya hapo kila kitu kikawa ovyo, nikaanza kuumwa, waliotaka kunioa, wote wakakimbia, kila mtu aniona sifai. Shangazi yangu alilitambua hilo, akaja kunichukua akanileta Dar es Salaam.

Lakini alihangaika kila kona. Kamaliza waganga wote, lakini hakuna kitu. Mwisho akajiamulia kukaa tu.” Alishuka pumzi kama mtu aliyechoka. “Na mimi sijui chochote masikini ya Mungu, nikakaa tu.

Ikitokea hali hii ya kitu chochote chenye harufu kali kama manukato, au udi napandisha, ndiyo huyo jini anakuja na anasema kabisa mimi ni wa kwake, nikiolewa kwa ndoa na mwanaume yoyote anatuua wote wawili.” “Sasa kwa nini ulikuja kwangu Nuru, ulitaka tufe wote nini?” Akauliza kama mzaha hivi, lakini alikuwa anamaanisha.

**“Mzee mimi ni msichana mdogo sana, wala sipendi haya madudu, yameniingia mimi mwenyewe nikiwa sijui. Na aliyesababisha haya yote ni mama wa kambo, hakuwa mtu mzuri kabisa...”**

“Nadhani mzee Raia alishasema hapa wiki iliyopita kuwa jini halina tatizo na mtu wa kupita, lenyewe halitaki tu niolewe, kumbuka aliyenitupia lengo nisiolewe tu, kwa hiyo wala usingekufa wewe wala mimi, labda ungenioa, lakini nilichosababisha ni ule udi uliochoma, yaani ndiyo ulikuwa umeliita.” “Du pole sana mama.” Heri alitoa pole “Ahsante.” Heri akamgeukia mzee Raia akamtazama usoni na kumuuliza. “Mzee sasa unatusaidiaje hapo, maana kila kitu ameshaeleza na kiko wazi.” Mzee alikohoa kidogo.

Akaingiza mkono kwenye kikapu chake kidogo alichokuja nacho. Akatoa vitu kadhaa ambavyo vilikuwa vigeni kwenye macho ya Heri na Nuru.

Akaviweka kwenye mkeka. Akafanya tena kwa mara ya pili. Alichokitoa sasa walikifahamu. Ni usinga. Muda wote huo, walikuwa kimya wakimtazama mzee raia akifanya vitu vyake.

“Kama nilivyokueleza wiki iliyopita, umetupiwa jini liitwalo Anzura. Umesema mwenyewe kuwa ni mama yako wa kambo.

Mtu aliyefanya hivyo, amekutupia jini ambalo ikimwingia binadamu linamzuia kuoa kwa mwanaume na kuolewa upande wa mwanamke. Wiki iliyopita nimelifafanua sana hili sina haja ya kulirudia sana.

Lenyewe linataka mtu afanye uhuni tu linapokuja suala la kuolewa mtihani. Nilikuahidi kukusaidia binti, sasa leo naifanya kazi hiyo.” Kimya kikaendelea ndani humo. Akatoa chupa ndogo, na kuifungua. Akamimina kimiminika mfamo wa mafuta hivi kwenye mfuniko wake, akamtaka atoke kitandani, akae kwenye mkeka. Nuru akatii. Akamminia kichwani. Akachukua mkebe na kufungua ndani ambamo kulikuwa na vitu kama unga hivi. Akachota na mkono wake akampaka kwenye paji la uso.

Kama vile haitoshi, akachukua kibuyu ambacho kilikuwa na mti hivi, ambao alipoutoa ulionekana kuwa na vitu kama asali au damu. Akampaka kwenye paji la usi, mabegani na kumtaka ageuke. Akampaka pia chini kidogo ya shingo yake. “Haya nenda kakae pale ulipokaa mwanzo, kitandani.”

Mzee Raia akaanza kuongea maneno ambayo hayakueleweka vema kwa wengine. Alitumia dakika mbili hivi.

“Nadhani mambo yatakuwa yamekamilika. Jini halitorudi tena. Nimelifukuza.

Kama ingekuwa wengine ningewaambia walete mbuzi, achinjwe ili damu yake apewe kama masharti ya kutorudi tena kwenye mwili wa binti huyu. Lakini nimeona kijana ungetumia gharama kubwa na ingechukua muda, maisha yenyewe ni magumu hata.

Nimeamua kulifukuza kwa nguvu.” Wote wawili walimshukuru mzee huyo ambaye aliwaambia hataki senti tano, ameamua kumsaidia binti huyo kutokana na heshima na adabu aliyokuwa nayo Heri.

“Kwa uthibitisho, nenda kanunue udi halafu uashe. Kama atapandisha basi litakuwa hakijaondoka, kama asipopandisha basi tumefanikiwa kuliondoa.”

*****************************

Dakika tano tu baadaye Heri alirejea na udi. Akauchomeka pale pale ambako wiki iliyopita alifanya hivyo.

“Haya uwashe sasa.” Mzee Raia akamwambia. Akatekeleza. Udi uliwaka, sekunde chacha baadaye moshi na harufu yake ilijaa chumba kizima. Hakukuwa na chochote kilichobadilika. Wote watatu waliendelea kupiga stori, zilizoanzishwa na mzee huyo, ili kuzima kile kilichoonekana Heri na Nuru walikuwa wakiuangalia sana kwa hofu.

Kwa sababu kila mmoja alikuwa anajua nini kilitokea wiki iliyopita. Dakika tatu zilipita bila chochote kutokea.

Robo saa baadaye, Nuru alinyanyuka ghafla na kumfuata mzee Raia, akamshika mikono yake akimtaka asimame. Aliposimama akamkumbatia kwa nguvu. Halafu kaangua kilio cha kwikwi. “Nyamaza Nuru.” Heri alibembeleza.

“Hapana. Muache alie. Akilia anapunguza uchungu alionao ndani ya moyo wake. Alikuwa na majonzi na mashaka.” Nuru alipomaliza kulia, dakika moja na nusu hivi, alijifuta machozi, mikono yake na mwili wake haikutoka kwa mzee Raia. “Mzee sijui niseme nini. Hili jambo limenitesa kwa muda mrefu, familia yangu hasa shangazi yangu. Amehangaika sana. Amepoteza pesa nyingi sana.


Shangazi yangu ni masikini sana, wakati mwingine hata kula yetu ni ya shida, lakini alipambana mpaka akashindwa. Leo hii ni kama ndoto kwangu, nimepona kirahisi sana. Naamini nimepona kwa sababu haijawahi kutokea nikakaa dakika zote hizi bila kupandisha.

Mimi ilikuwa ikinipata harufu ya manukato tu, hasa udi, napandisha hapo hapo, muulize Heri atakuambia. Sijui nikupe zawadi gani mzee, ila naomba uwe kama mzazi wangu kuanzia leo.”

“Nilikuambia binti yangu siku ile kuwa nitakusaidia bure. Na hii ni kwa sababu ya huyu mwenzako. Ni rafiki yangu sana na yeye hakuona mtu mwingine wa kumsaidia akanitafuta. Wala halina tatizo, wewe na huyu mwenzako, wote ni kama wanangu tu. Na kwa hili nadhani tutakuwa karibu sana.

Nahitaji pia kumuona huyu shangazi yako.” “Yaani baba, nikirudi na kumwambia hili sijui atacheza ngoma gani. Sijui atapika chakula gani shangazi yangu jamani.

ITAENDELEA JUMAPILI





# HARMONIZE ATAMANI KUINGIA BILLBOARD

MKURUGENZI wa lebo ya Konde Music Worldwide, Rajab Kahali maarufu kama Harmonize, amesema mawazo yake ni kuingia katika chati maarufu ya muziki duniani ya Billboard, na kushika nafasi za mwanzo.

Harmonize amesema licha ya kuwa na elimu ya darasa la saba, lakini ujasiri wake ndio ambao umemfanya kujisukuma na kukutana na baadhi ya mastaa wakubwa kutoka Marekani akiwemo Bobby Shmurda.

"Vitu ambavyo nimevipitia kwenye maisha yangu vinanifanya niamini kwamba mtu unaweza kuwa chochote utakachokuwa. Mimi sijawahi kata tamaa. Ukiniuliza hapa ninawaza kutinga katika nafasi ya kwanza kwenye Billboard, na hilo ni suala la muda tu, naamini inawezekana," amesema.



# Diamond, Darule kuja na kolabo

MWANAMUZIKI maarufu wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz, ameonyesha umwamba wake baada ya kupata dili la kufanya kolabo na staa wa Marekani Jason Darule.

Diamond alionyesha mawasiliano kati yake na Darule, ambayo mwanamuziki alimuomba kufanya naye kazi, na bila kusita mkali huyo alimkubalia na kumtaka amtumie demo ya wimbo husika.

Kama dili hilo litafanikiwa itakuwa ushindi kwa muziki wa Bongo Fleva na kufungua milango kwa wasanii wengine kupata mialiko ya ushirikiano na wasanii wakubwa wa nchi hiyo.



## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### GREENWOOD ANUKIA LAZIO

LAZIO imeanza mazungumzo na Manchester United kuhusu uhamisho wa pauni milioni 30 ili kumnunua mshambuliaji wa zamani wa Timu ya Taifa ya England, Mason Greenwood, mwenye umri wa miaka 22. ***(Mail)***

#### JUVENTUS, NAPOLI VITANI

JUVENTUS na Napoli pia zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili nyota wa zamani wa England, Mason Greenwood. ***(Independent)***

#### BRUNO SOKONI ENGLAND

ARSENAL wanaweza kutafuta ofa ya kumtoa mchezaji pamoja na fedha ili kumnunua kiungo wa kati wa Newcastle na Timu ya Taifa ya Brazil, Bruno Guimaraes, mwenye umri wa miaka 26. ***(Football Transfers)***

#### OLISE AGOMBEWA EPL

LIVERPOOL inalenga kuzishinda Chelsea na Manchester United katika mbio za kumsajili winga Mfaransa, Michael Olise mwenye umri wa miaka 22, kutoka Crystal Palace ***(Football Transfers)***

#### MC KENNIE AKARIBIA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur wamewatangulia Aston Villa katika harakati za kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Marekani, Weston McKennie, mwenye umri wa miaka 25 kutoka Juventus . ***(Football Insider)***

#### WILLIAMS AICHAGUA BARCA

WINGA wa Athletic Bilbao, Nico Williams mwenye umri wa miaka 21, anaendelea kushikilia uwezekano wa kuhamia Barcelona licha ya kuwa na mazungumzo na Aston Villa, Arsenal, Liverpool na Newcastle United ***(HITC)***

#### CASH KUMRITHI DUMFRIES

MATTY Cash wa Aston Villa tayari anafuatiliwa na AC Milan lakini sasa wapinzani wao Inter Milan wanamfikiria beki huyo wa kulia wa Poland mwenye umri wa miaka 26, kama anaweza kuziba nafasi ya mlinzi wa Uholanzi, Denzel Dumfries (28). ***(Sky Sport Italia)***

#### WALSH AKARIBIA ARSENAL

KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Keira Walsh, mwenye umri wa miaka 27, anakaribia kujiunga na Arsenal. ***(90min)***

#### CHELSEA KUSAJILI STRAIKA

CHELSEA inavutiwa na mshambuliaji wa Atletico Madrid, Samu Omorodion na straika wa Aston Villa na Timu ya Taifa ya Colombia, Jhon Duran, lakini watamsajili mmoja tu wa wachezaji hao wenye umri wa miaka 20. ***(Fabrizio Romano)***

#### DAGUR KUTUA NEWCASTLE

NEWCASTLE United imeonyesha nia ya kumsajili winga wa Timu ya Taifa ya Iceland, Jon Dagur Thorsteinsson, 25, ambaye anaichezea Klabu ya OH Leuven ya Ubelgiji. ***(Chronicle Live)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# PULISIC : MAREKANI IKO TAYARI COPA AMERICA

**DALLAS,** Marekani

CHRISTIAN Pulisic amesema uzoefu uliopatikana wa Timu ya Taifa ya Marekani katika miaka kadhaa iliyopita uko tayari kufikia kiwango cha juu cha mafanikio, kuanzia mashindano ya Copa América 2024.

**Marekani itafungua michuano hiyo, ambayo inaandaa kwa mara ya pili leo dhidi ya Bolivia.**

Na Pulisic ana nia ya kuwa mechi hiyo iwe mwanzo wa kuonyesha ulimwengu maendeleo ambayo timu yake imefikia.

"Sasa ni wakati wa kujithibitisha," alisema fowadi huyo akiwaambia

**●●● Mshambuliaji huyo atamba wana uwezo wa kubeba kombe...**

waandishi wa habari hapo juzi.

"Nadhani tumejifunza mengi. Tumefanya vyema katika Kombe la Dunia. Tumewaonyesha watu, sawa, timu hii inaweza kucheza.

"Na sasa inahusu sio tu kuweka maonyesho hayo, lakini kutafuta njia ya kupata matokeo katika mechi kubwa zaidi. Hiyo ni hatua inayofuata kwetu."

Ikizingatiwa ataingia uwanjani katika mechi ya leo, hii itakuwa mara ya pili kwa Pulisic kucheza Copa América, baada ya kupamba uwanja katika mechi tatu mwaka 2016.

Katika mashindano hayo, Pulisic alikuwa akiingia akitokea benchi, lakini sasa yeye ni mhimili mkuu na anachuliwa kuwa mmoja wa viongozi.

"Kwangu mimi, ni muhimu sana kuongoza kwa jinsi ninavyojiendesha kila siku katika mazoezi," alisema.

"Pia ninachofanya uwanjani, kwenye mchezo na kuwaonyesha hivyo.

# OLISE ACHAGUA KUTUA BAYERN




**LONDON,** England

MICHAEL Olise ameamua kujiunga na Bayern Munich baada ya Chelsea kujiondoa katika kinyang'anyiro cha kuwania saini yake, ripoti imefichua.

The Blues wanawinda wachezaji kadhaa wapya wa nafasi ya ushambuliaji msimu huu wa joto na walikuwa wamemlenga Olise, wakifanya mazungumzo na Mfaransa huyo na klabu yake ya Crystal Palace.

Hata hivyo, kama ilivyofichuliwa na The Athletic, dili halitafanyika kwa sababu Chelsea wamejiondoa kwenye meza ya mazungumzo.

inasemekana fedha zilizohitajika kumsajili Olise kwa Chelsea zilikuwa nyingi na wameamua kutofuata makubaliano.

Badala yake, Olise amekubali kujiunga na Bayern Munich, ambao walipewa ruhusa ya kuzungumza na Mfaransa huyo na wanatarajiwa kukubaliana na Crystal Palace katika siku zijazo.

Chelsea ina mpango wa kuwazawadia wachezaji wao wa sasa, badala ya kutoa fedha nyingi kwa wachezaji wapya waliosajiliwa, lakini bado wana nia ya kufanya usajili ili kuimarisha safu ya ushambuliaji iliyoko chini ya Kocha, Enzo Maresca.

Chelsea pia wanaaminika wanahitaji winga mpya lakini itabidi waamue walengwa wapya wa kipaumbele baada ya kuamua dhidi ya kuendeleza nia yao ya kumnunua Olise.

# 'Uholanzi tumenyimwa bao'



**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA wa Uholanzi, Ronald Koeman, amesema mwamuzi alifanya makosa kwa kukataa bao la timu yake dhidi ya Ufaransa kwenye michuano ya Ulaya lakini akaongeza pande zote mbili zilifurahia pointi katika suluhu ya mechi ya Kundi D iliyochezwa juzi usiku.

Bao la kipindi cha pili kutoka kwa Xavi Simons lilikataliwa kwa sababu Denzel Dumfries, akiwa ameotea karibu na kipa, Mike Maignan, aliadhibiwa na uamuzi huo kuthibitishwa na VAR baada ya kuchelewa kwa muda mrefu.

Lakini Koeman alisema alitazama picha za tukio hilo baadaye na hakukubaliana na mwamuzi, Anthony Taylor.

"Nafasi ya Dumfries ni ya kuotea, hiyo ni kweli. Lakini hakumsumbua kipa. Na hilo lisipofanyika basi ni bao kisheria kwa maoni yangu," alisema kocha huyo wa Uholanzi wakati wa mkutano na wanahabari baada ya mechi.

"Je, walihitaji dakika tano kuiangalia kwa sababu ni ngumu sana?" Koeman aliongeza.

Lakini mkwamo wa kutofungana ulikuwa matokeo ya kuridhisha kwa pande zote mbili.

Ingawa nadhani bao lilipaswa kusimama, hatua yangu kutoka kwa hili ni matokeo ya haki.

"Naweza kukubali hili, ingawa kulikuwa na wakati wa mchezo ambapo hatukuwa tayari kuanza na pengine ni kutokana na ukweli tulikuwa tunapambana na mpinzani mkubwa Ufaransa.

# CAF yatangaza AFCON kuanza Desemba 2025

**CAIRO,** Misri

FAINALI za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), sasa zitachezwa kuanzia Desemba 21, mwaka 2025 hadi Januari 18, mwaka 2026, Shirikisho la Soka la Afrika (CAF), limetangaza.

Mashindano ya 2025 nchini Morocco yalipaswa kufanyika katikati ya mwaka lakini yamebadilishwa kwa sababu ya Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), kupanua Kombe la Dunia la klabu.

CAF pia imesogeza fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wanawake mwaka huu kwa miezi 12 hadi kuanzia Julai 5 hadi 26, mwakani. Pia itafanyika Morocco.

Tarehe za michuano hiyo miwili zimekuwa zikitazamiwa kwa hamu kwa sababu CAF hapo awali ilikubali kutatizika na kalenda ya kimataifa iliyojaa watu wengi.

"Kutangazwa kwa tarehe za AFCON nchini Morocco 2025 kulichukua muda mrefu zaidi kuliko ilivyotarajiwa, kwa sababu kulikuwa na mijadala tata na wakati fulani yenye changamoto na wahusika mbalimbali, kwa kuzingatia kalenda ya mechi za kimataifa na za ndani," alisema Rais wa CAF, Patrice Motsepe.

"CAF imejitolea kulinda na kuendeleza maslahi ya wachezaji wa Kiafrika, ambao wanacheza katika klabu barani Ulaya na duniani kote.

CAF pia imejitolea kujenga uhusiano wenye manufaa kwa mashirikisho mengine ya soka na FIFA," aliongeza.

Kushiriki katika michuano ya AFCON katikati ya msimu wa Ligi ya Ulaya kunasababisha hali ya sintofahamu kwa wachezaji wa Kiafrika wenye makazi yao Ulaya, ambao wanapaswa kuamua kati ya klabu au nchi.

Ili kupunguza hili, CAF hapo awali iliamua fainali zingesogezwa katikati ya mwaka, kila mwaka usio wa kawaida, kuanzia 2019 na kuendelea.

Lakini tangu michuano ya katikati ya mwaka iliyofanyika Misri mwaka 2019, bodi inayosimamia soka Afrika imerejea na uamuzi wao na kuandaa fainali mbili zilizopita nchini Cameroon na Ivory Coast mwanzoni mwa mwaka.



## Usajili Chama sinema ile ile

INATOKA UK. 24

na uongozi yalianza tena, yamekwenda vizuri, maslahi ya mchezaji yamezingatiwa, ninachokwambia mpaka sasa bado hajasaini mkataba, ila ameridhia kubaki, kinachosubiriwa ni saini, dole gumba na kuanza kupiga picha ya utambulisho," kiliongeza chanzo hicho.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesema hakuna mchezaji anayetakiwa kubaki na klabu hiyo ataondoka.

Ahmed alisema Kamati ya Usajili inajipanga kuimarisha kila idara katika kikosi chao kwa ajili ya kuongeza nguvu na kufikia malengo kwenye msimu mpya wa mashindano.

"Ukiona mchezaji yoyote wa Simba ameondoka ujue hatumhitaji, kama yupo kwenye malengo yetu hawezi kuondoka," alisema ofisa huyo.

Aliongeza wako katika hatua za mwisho za kukamilisha wachezaji wanaowahitaji pamoja na kutangaza kocha mkpya ambaye ataongoza benchi la ufundi la timu hiyo.

Tayari Simba imeshatangaza itaenda kuweka kambi kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya katika mji wa Ismailia, ulioko Misri ukiwa na kikosi kamili.

## Simba yaibomoa Mashujaa FC

INATOKA UK. 24

ubora mkubwa.

"Bado tunahitaji beki mwingine, tunahitaji watu wa kazi kweli kweli, tumempata Lameck Lawi, tunaye Fondoh Che Malone, pia yupo kijana, Hussein Kazi, sasa tunahitaji mlinzi mwingine wa kimataifa ili wawe wanne kwa lengo la kuimarisha ulinzi zaidi msimu ujao," alisema Ahmed.

Alisema lengo la kumsajili Lawi, ni kuifanya timu hiyo ipunguze idadi ya mabao ya kufungwa kwa sababu msimu uliopita iliruhusu magoli mengi kwa mara ya kwanza baada ya misimu kadhaa kupita.

"Kuondoka kwa Kennedy, kunafungua milango ya kijana mwingine wa Kitanzania kutoka Coastal Union anayeitwa Lawi kuonekana, tuko katika mipango ya kuitengeneza Simba imara na thabiti, kumbuka msimu uliomalizika Simba imeruhusu mabao mengi sana, kulikuwa 'kunavuja' sasa huyo na mwingine atakayetua, wanakuja kuziba eneo hilo ili irudi ile Simba inayoruhusu mabao machache, " alisema.

# JKU YATWAA UBINGWA WA LIGI KUU ZANZIBAR

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya JKU SC imetwaa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu wa mwaka 2023/2024 baada ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Kipanga katika mechi ya kufunga pazia la ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Amaan juzi.

Kwa matokeo hayo, JKU ilifikisha pointi 66 na kukaa kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ambayo ilishirikisha timu 16 kutoka Pemba na Unguja.

nafasi ya pili katika ligi hiyo ilichukuliwa na Zimamoto yenye pointi 62 huku KMKM yenye pointi 57 ilimaliza ya tatu na KVZ ilikamilisha 'Top Four' ikiwa na pointi 56.

**Wakati JKU wakifurahia, Kundemba iliungana na timu za Ngome, Maendeleo na Jamhuri kushuka daraja.**

Mechi tano zilichezwa juzi katika viwanja vya Finya na Gombani vilivyoko Pemba wakati upande wa Unguja, michezo ya mwisho ilifanyika kwenye Uwanja wa Mau na Amaan.

Kundemba yenyewe ilicheza mchezo wake wa mwisho kwenye Uwanja wa Mao Zedong ambapo ilipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Malindi SC, matokeo ambayo hayakuwasaidia kujinusuru na janga la kushuka daraja wakati New City walipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Zimamoto.

KVZ ilimaliza ligi hiyo kwa ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Jamhuri, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Funya huku Hard Rock ikiwaadhibu Maendeleo United kwa mabao 4-1, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Gombani.

Kundemba iliyojikusanyia pointi 35 ilimaliza kwenye nafasi ya 13 katika msimamo wa ligi hiyo ikifuatiwa na Ngome yenye alama 27 wakati Jamhuri wamemaliza msimu wakiwa na pointi 20 na Maendeleo waliburuza mkia kutokana na kujikusanyia alama 15 tu kwa msimu mzima.

JKU rasmi sasa itaiwakilisha Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao huku Chipukizi ya Pemba, ambao ni mabingwa wa Kombe la ZFF (Shirikisho la Soka Zanzibar), wamekata tiketi ya kushiriki michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.



Mchezaji wa mpira wa kikapu wa Vijana, Evarest Matiko (aliyeruka juu), akijaribu kufunga huku akizongwa na wachezaji wenzake katika mazoezi ya timu hiyo yaliyofanyika kwenye Uwanja wa JMK Park, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Wachezaji wa Gofu kuchuana Julai Dar*

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya wazi ya gofu yamepangwa kufanyika Julai 5 hadi 7, mwaka huu kwenye viwanja vya Klabu ya Lugalo, Dar es Salaam imeelezwa.

Akizungumza jijini jana, Mwenyekiti wa Klabu ya Gofu Lugalo, Brigedia Jenerali Mstaafu, Michael Luwongo, alisema shindano hilo litashirikisha klabu mbalimbali kutoka Tanzania Bara.

Luwongo alisema lengo la mashindano hayo ni kuwafanya wachezaji wapate nafasi ya kuonyesha viwango vyao lakini pia kuboresha mahusiano baina ya watu mbalimbali watakaoshiriki.

"Shindano hili litakuwa la aina yake kwa sababu mpaka sasa idadi kubwa ya washiriki wameanza kujiandikisha ili kuonyesha nia ya ushiriki wao, ninaamini kila klabu itaonyesha upinzani mkubwa," alisema Luwongo.

Alisema mashindano hayo yatakuwa na makundi matatu ambayo ni watoto, wanawake na wachezaji wakongwe.

Naye Rais wa Chama cha Gofu Tanzania (TGU), Gilman Kasiga, alisema wachezaji watakaofanya vizuri watapata nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa huku akiwashukuru wadau waliojitokeza katika kusaidia maandalizi.

"Mchezo wa gofu kwa sasa umeshika kasi tofauti na miaka iliyopita, kuna idadi kubwa ya Watanzania wanajiunga, tunaamini sisi TGU pia itatusaidia kupata wachezaji watakaoiwakilisha nchi katika mashindano mbalimbali yaliyoko mbele yetu," Kasiga alisema.

# Michezo

Jumapili Juni 23, 2024

Nipashe




**Olise achagua kutua Bayern** UKURASA 22

# USAJILI CHAMA SINEMA ILE ILE

## ●●● Yanga yawataka watani zao waache hofu, wanayemtaka hachomoi...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mchakato wa usajili wa wachezaji wa ndani na nje ya Tanzania kuelekea maandalizi ya msimu mpya ukiendelea, unaweza kusema Wekundu wa Msimbazi wanawachelewesha watani zao, Yanga kumtangaza kiungo, Clatous Chama, ametua katika timu yao, imeelezwa.

Chama amekataa kusaini mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia Simba kwa sababu hawajafikia kiwango cha fedha ambacho amekihitaji wakidai hastahili kulipwa kutokana na umri na kiwango chake cha sasa huku tetesi zikieleza Mzambia huyo tayari ameshamalizana na Yanga.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, amesema wanachelewa kutangaza majina ya wachezaji walioachwa na wapya ambao wamewasajili kutokana na baadhi ya klabu kutokamilisha mchakato wa kuachana na nyota wao.

**Kamwe bila kutaja majina, alisema kuna klabu zinachelewa kuwapa barua za 'kwaheri' nyota wao kwa hofu ya kujiunga na Yanga na hali hiyo imezua wasiwasi kwa wanachama na mashabiki wa Simba hasa wapi anakwenda kiungo huyo.**

"Kuna mchezaji mmoja anamaliza mkataba, lakini jamaa hawataki kumpa barua, wana hofu atakuja kwetu, wampe tu kijana wa watu ili aje kwenye klabu ya ndoto yake, na hilo ndilo limetufanya mpaka sasa tuahirishe au tuchelewe kuwapa 'Thank You' tutakaoachana nao na kutangaza wachezaji wapya ambao tumewasajili," alisema Kamwe.

Taarifa kutoka Simba zinasema mkataba wa Chama na Simba umebakiza siku chache na sasa kanuni zinamruhusu kufanya mazungumzo na timu yoyote inayohitaji huduma yake.

"Mkataba wa Klabu ya Simba na Chama unamalizika ifikapo Juni 30, na baada ya hapo anakuwa huru, ameshazungumza na Yanga, pande zote mbili zimekubaliana wanasubiri mkataba wake uishe ndiyo atie wino, ameshakubaliana nao ada ya usajili na mshahara na posho nyingine muhimu, kinachosubiriwa ni muda tu," kilisema chanzo chetu.

Chanzo hicho kiliendelea kusema huenda 'upepo' ukabadilika na Chama ambaye hii si mara ya kwanza anahusishwa kutua Jangwani, anaweza kubakia Msimbazi na 'kuzika' ndoto za Yanga kupata huduma ya mchezaji huyo.

"Awali hawakufikia mwafaka na Chama, lakini mmoja wa Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi kutoka upande wa mwekezaji ambaye pia yumo katika Kamati ya Usajili ameliingilia kati suala hilo.

Siku mbili zilizopita, mazungumzo kati ya Chama

INAENDELEA UK. 23




Chama

# Simba yaibomoa Mashujaa FC



Omary- straika Mashujaa

**Na Adam Fungamwango**

HUKU ikiwa katika mchakato wa kusaka beki mpya wa kati ili kurithi mikoba ya Mkongomani Henock Inonga, Simba inatajwa imekaribia kumsajili mshambuliaji wa Mashujaa FC, Omari Omari, taarifa za ndani zimeeleza.

Inonga, alikuwa na mkataba na Simba hadi Juni, mwakani, anatajwa kujiunga na FAR Rabat ya Morocco.

Tayari Simba imemtangaza beki wa kati kutoka Coastal Union, Lameck Lawi, ambaye anaziba pengo la Kennedy Juma, timu hiyo bado haijapata mbadala wa Inonga ambaye hatakuwa sehemu ya kikosi chao katika msimu mpya.

Taarifa za ndani za Simba zinadai klabu hiyo iko katika mazungumzo na beki wa kati wa Asec Mimosas ya Ivory Coast, Anthony Tra Bi Tra.

"Naweza kukwambia muda wowote tunaweza kukamilisha dili hilo na kumtangaza, ni mchezaji mzuri, yeye na Adam Adam, waliisaidia sana Mashujaa kubaki Ligi Kuu baada ya kusajiliwa kipindi cha dirisha dogo la usajili," alisema mtoa taarifa.

Mbali na mchezaji hiyo, Simba pia inapambana kuhakikisha inapata saini ya beki wa kushoto wa KMC, Rahim Shomari, ili kuja kusaidiana na Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr.'

Chanzo hicho kimesema Rahim ambaye makuzi yake yalianzia katika kikosi cha vijana cha Simba, anatajwa kurejea nyumbani na KMC imesema itakuwa tayari kumruhusu kuondoka itakapolipwa Sh. milioni 100.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally (pichani), aliiambia gazeti hili bado wako katika mazungumzo na beki mwingine kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kucheza katika nafasi ya ulinzi.

Ahmed alisema wanajipanga kuwa na mabeki wanne watakaocheza katika nafasi hiyo na wanaamini watakuwa ni wazoefu na wenye

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >